**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

Budget Documents MoFP Budget

2018-06

# Hotuba ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Makadirio ya Mapato na matumizi 2018-2019

Tanzania, Jamhuri ya Muungano

Wizara ya Fedha na Mipango

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/230

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

# HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO MHE. DKT. PHILIP I. MPANGO (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA 2018/19

“*Kodi ni kitu muhimu. Lazima kila mtu anayestahili kulipa kodi alipe*”

Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

20 Novemba, 2015

# YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI ... 1
2.0 MAJUKUMU YA WIZARA ... 4
3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2017/18 ... 6
3.1 MAPATO KWA MWAKA 2017/18 ... 7
3.2 MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA 2017/18 ... 7
3.3 MATUMIZI KWA AJILI YA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/18 ... 9
3.4 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA 2017/18 ... 10
3.4.1 Kubuni na kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla ... 10
3.4.2 Uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ... 11
3.4.3 Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini ... 13
3.4.4 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali ... 15
3.4.5 Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ... 18
3.4.6 Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma ... 20
3.4.7 Usimamizi wa Malipo ... 25
3.4.8 Deni la Serikali ... 26
3.4.9 Usimamizi wa Mifumo ya Taarifa za Kifedha ... 29
3.4.10 Usimamizi wa Mali za Serikali ... 31
3.4.11 Ununuzi wa Umma ... 32
3.4.12 Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ... 36
3.4.13 Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma ... 37
3.4.14 Mafao ya Wastaafu na Mirathi ... 40
3.4.15 Udhibiti wa Utakasishaji Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi ... 42
3.4.16 Tume ya Pamoja ya Fedha ... 44
3.4.17 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) ... 44
3.5 USIMAMIZI NA URATIBU WA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA CHINI YA WIZARA ... 47
3.5.1 HUDUMA ZA KIBENKI ... 47
3.5.2 Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ... 56
3.5.3 Rufani za Kodi ... 58
3.5.4 Huduma za Bima ... 59

3.5.5 Mitaji na Dhamana ... 61
3.5.6 Dhamana za Uwekezaji Tanzania ... 68
3.5.7 Taasisi za Mafunzo ... 70
3.5.8 Taasisi za Kitaalam na Huduma Nyinginezo ... 74
3.5.9 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo mwaka 2017/18 ... 79
3.6 CHANGAMOTO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA ... 82
3.6.1 CHANGAMOTO ... 82
3.6.2 HATUA ZA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO ... 83
4.0 MALENGO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2018/19 ... 84
4.1 MPANGO WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA ... 85
4.1.1 Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Uchumi Jumla ... 85
4.1.2 Uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ... 86
4.1.3 Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini ... 87
4.1.4 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali ... 89
4.1.5 Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ... 92
4.1.6 Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma ... 94
4.1.7 Usimamizi wa Malipo ... 95
4.1.8 Deni la Serikali ... 96
4.1.9 Mchango wa Mwajiri (Serikali) kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ... 96
4.1.10 Usimamizi wa Mifumo ya Taarifa za Kifedha ... 97
4.1.11 Usimamizi wa Mali za Serikali ... 98
4.1.12 Ununuzi wa Umma ... 98
4.1.13 Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ... 101
4.1.14 Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma ... 102
4.1.15 Mafao ya Wastaafu na Mirathi ... 104
4.1.16 Udhibiti wa Utakasishaji Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi ... 105
4.1.17 Tume ya Pamoja ya Fedha ... 106
4.1.18 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ... 106
4.1.19 Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma ... 107
4.1.20 Mradi wa Kimkakati wa kuongeza mapato kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa (Strategic Revenue Generation in LGAs Project) ... 109

4.2 USIMAMIZI NA URATIBU WA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA CHINI YA WIZARA ........ 109
4.2.1 Huduma za kibenki ........ 109
4.2.2 Rufani za Kodi ........ 113
4.2.3 Huduma za Bima ........ 113
4.2.4 Mitaji na Dhamana ........ 115
4.2.5 Dhamana za Uwekezaji Tanzania ........ 118
4.2.6 Taasisi za Mafunzo ........ 119
4.2.7 Taasisi za kitaalam na Huduma nyinginezo ........ 122
5.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/19 ........ 127
5.1 MAKADIRIO YA MAPATO ........ 127
5.2 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/19 ........ 128
5.2.1 FUNGU 50 – WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO ........ 129
5.2.2 FUNGU 21 - HAZINA ........ 130
5.2.3 FUNGU 22- DENI LA TAIFA ........ 131
5.2.4 FUNGU 23 – MHASIBU MKUU WA SERIKALI ........ 131
5.2.5 FUNGU 7 – OFISI YA MSAJILI WA HAZINA ........ 132
5.2.6 FUNGU 10 – TUME YA PAMOJA YA FEDHA ........ 133
5.2.7 FUNGU 13 – KITENGO CHA KUDHIBITI FEDHA HARAMU ........ 133
5.2.8 FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI ........ 134
6.0 SHUKRANI ........ 135
7.0 VIAMBATISHO ........ 136

## 1.0 UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa Hoja kwamba, Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2017/18 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka ujao wa fedha 2018/19.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2018/19.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda nitumie fursa hii kuwapongeza Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim M. Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Taifa letu kwa ujasiri na uzalendo wa hali ya juu.

Mwenyezi Mungu azidi kuwapa afya njema, hekima na busara katika kuliongoza Taifa letu.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendesha vema majadiliano ya bajeti za Wizara mbalimbali kwa mwaka 2018/19. Aidha, napenda kumpongeza Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, (Mb.) kwa kuchaguliwa tena pamoja na Makamu Mwenyekiti mpya Mhe. Jitu Vrajlal Soni (Mb.) kuiongoza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Aidha, nawapongeza na kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa maoni, ushauri na mapendekezo waliyotoa ambayo yamesaidia sana katika kuboresha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka 2018/19.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie pia fursa hii kuwapongeza Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro - Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini, Mhe. Justin Monko – Mbunge wa Singida Kaskazini, Mhe. Dkt. Stephen Kiruswa - Mbunge wa Jimbo la Longido, Mhe. Dkt. Godwin Mollel - Mbunge wa Jimbo la Siha na Mhe. Maulid Mtulia - Mbunge wa Jimbo la Kinondoni kwa kuchaguliwa kuwa wabunge katika Bunge lako Tukufu. Aidha, natoa pole kwa Bunge

lako Tukufu kwa kuwapoteza Mhe. Leonidas Gama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini na Mhe. Kasuku Samson Bilago aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Buyungu. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji - Mbunge wa Kondoa na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa ushirikiano anaonipatia katika kuhakikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango unafanikiwa. Aidha, nawashukuru Bw. Doto James - Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu Bibi Amina Kh. Shaaban, Dkt. Khatibu M. Kazungu na Bi. Susana Mkapa kwa kusimamia shughuli za kila siku za kiutendaji za Wizara yangu kwa juhudi kubwa. Pia napenda kumpongeza kwa dhati Prof. Florens Luoga - Gavana mpya wa Benki Kuu ya Tanzania na kumshukuru yeye pamoja na Bw. Charles Kichere - Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kwa kusimamia kwa weledi taasisi nyeti walizokabidhiwa. Taasisi hizi zinatoa mchango mkubwa sana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Nawashukuru pia, Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi zote zilizoko chini

ya Wizara, Wakuu wa Vitengo na wafanyakazi wote wa Wizara, kwa kutimiza wajibu wao vema wa kuwatumikia Watanzania.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya utangulizi huo, yafuatayo ni maelezo ya majukumu ya Wizara, mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka 2017/18 na malengo kwa Mwaka 2018/19.

## 2.0 MAJUKUMU YA WIZARA

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Namba 144 la tarehe 22 Aprili, 2016, yafuatayo ni majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango:-

i. Kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za fedha, mapato na matumizi, ununuzi wa umma, ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
ii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mipango na Miongozo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo;
iii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya Mipango ya Taifa ya Maendeleo;
iv. Kusimamia utekelezaji wa Mashirika na Taasisi za Umma;

v. Kuandaa miongozo ya Bajeti ya Serikali;
vi. Kuandaa Bajeti ya Serikali na kusimamia utekelezaji wake;
vii. Kusimamia masuala ya ushirikiano wa kifedha wa kimataifa;
viii. Kudhibiti biashara ya fedha haramu pamoja na ufadhili wa ugaidi;
ix. Kusimamia ulipaji wa mafao na pensheni ya wastaafu;
x. Kusimamia na kudhibiti mali na vifaa vya serikali;
xi. Kufanya ukaguzi wa ndani na wa nje wa hesabu za Serikali;
xii. Kutunza na kusimamia mali za adui;
xiii. Kusimamia na kudhibiti Deni la Taifa, Mikopo na Dhamana;
xiv. Kuratibu utekelezaji wa sera ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
xv. kusimamia masuala ya Tume ya Pamoja ya Fedha;
xvi. Kuratibu masuala ya uzalishaji;
xvii. Kusimamia na kudhibiti Masoko ya Mitaji na Dhamana;
xviii. Kuratibu takwimu za Taifa;
xix. Kusimamia maendeleo ya Sekta jumuishi ya Kifedha;

xx. Kufuatilia utekelezaji wa mipango ya kupunguza umaskini katika sekta mbalimbali;

xxi. Kusimamia masuala ya Watumishi chini ya Wizara;

xxii. Usimamizi na uratibu wa Taasisi na Mashirika ya Umma chini ya Wizara;

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2017/18

**9.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara imetekeleza majukumu yake kupitia mafungu tisa ya kibajeti pamoja na Taasisi na Mashirika 36 yaliyo chini yake **(Jedwali Na. 1)**. Mafungu hayo ni Fungu 50-Wizara ya Fedha na Mipango, Fungu 21-Hazina, Fungu 22-Deni la Taifa, Fungu 23-Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu 10-Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13-Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu, Fungu 7- Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 66-Tume ya Mipango na Fungu 45-Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

## 3.1 MAPATO KWA MWAKA 2017/18

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli ya jumla ya **shilingi bilioni 522.34** kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi ya pango, mauzo ya leseni za minada, gawio, marejesho ya mikopo, michango ya asilimia 15 ya pato ghafi la mashirika ya umma, mawasilisho kutoka Mfumo wa Kudhibiti Mawasiliano ya simu na marejesho ya mitaji iliyozidi kutoka katika taasisi na mashirika ya umma. Hadi Aprili, 2018 jumla ya **shilingi bilioni 655.71** zilikusanywa kutokana na vyanzo hivyo sawa na asilimia **125.5** ya lengo la mwaka. Ongezeko hili limetokana na ziada ya gawio kutoka Benki Kuu ya Tanzania, ambalo lilikuwa shilingi bilioni 300 ikilinganishwa na shilingi bilioni 180 ya makadirio.

## 3.2 MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA 2017/18

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Wizara ya Fedha na Mipango kwa mafungu yote tisa (9) iliidhinishiwa na Bunge kutumia jumla ya **shilingi 10,318,141,232,511 (bilioni**

**10,318.14)** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, **shilingi 89,847,360,068 (bilioni 89.85)** zilikuwa kwa ajili ya mishahara, **shilingi 766,860,872,443 (bilioni 766.86)** zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na **shilingi 9,461,433,000,000 (Bilioni 9,461.43)** zilikuwa kwa ajili ya kulipia Deni la Serikali na huduma nyingine.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2018 jumla ya **shilingi 8,542,019,747,533.57** (**bilioni 8,542.02**) zilitumika, sawa na asilimia 83 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya hizo, **shilingi 33,880,326,648.93** (**bilioni 33.88**) ni kwa ajili ya mishahara, sawa na asilimia **38** ya bajeti ya mishahara iliyoidhinishwa; na **shilingi 8,508,139,420,884.64** (**bilioni 8,508.14**) ni kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 83 ya bajeti ya matumizi mengineyo iliyoidhinishwa **(Jedwali Na. 2).** Matumizi ya mishahara yapo chini kutokana na fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya marekebisho ya mishahara ya watumishi wa Serikali kutokutumika kama ilivyokuwa imepangwa.

## 3.3 MATUMIZI KWA AJILI YA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2017/18

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa fedha za maendeleo, jumla ya **shilingi 1,429,083,949,741 (bilioni 1,429.08)** ziliidhinishwa kutumika kwa mafungu yote tisa. Kati ya fedha hizo, jumla ya **shilingi 1,382,975,800,000 (bilioni 1,382.98)** ni fedha za ndani na **shilingi 46,108,149,741 (bilioni 46.11)** ni fedha za nje. Hadi kufikia Aprili, 2018 jumla ya **shilingi 81,256,811,336.42 (bilioni 81.25)** zimetumika. Kati ya fedha hizo, **shilingi 53,481,878,307 (bilioni 53.48)** ni fedha za ndani na **shilingi 27,774,933,029.42 (27.77)** ni fedha za nje **(Jedwali Na. 3).**

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi ya maendeleo iliyotekelezwa ni pamoja na: Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma; Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Kuimarisha na Kuboresha Takwimu Tanzania (TSMP); Upanuzi wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini; na Kusaidia Ufanisi wa Bajeti za Wizara na Idara za Serikali (MDAs Performance Budget Support).

### 3.4 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA 2017/18

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba sasa kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2017/18.

#### 3.4.1 Kubuni na kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla

**16.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza jukumu hili, Wizara imejikita katika kuhakikisha kuwa kuna usimamizi wa malengo ya ukuaji wa uchumi, mfumuko wa bei, na mapato na matumizi ya Serikali. Katika mwaka 2017, kasi ya ukuaji wa uchumi imeendelea kuwa ya kuridhisha na kufikia wastani wa asilimia 7.1 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2016. Ukuaji huo ulichangiwa na kasi kubwa ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika sekta ya madini na uchimbaji mawe (asilimia 17.5), sekta ya maji (asilimia 16.7), sekta ya uchukuzi na uhifadhi mizigo (asilimia 16.6) na sekta ya habari na mawasiliano ambayo ilikua kwa asilimia 14.7.

17. ***Mheshimiwa Spika***, wastani wa mfumuko wa bei kwa mwaka 2017 ulikuwa asilimia 5.3 na umeendelea kupungua hadi kufikia asilimia 3.8 mwezi Aprili, 2018. Kupungua kwa mfumuko wa bei kulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula, utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu za kigeni, kuimarika kwa uzalishaji wa umeme, utekelezaji thabiti wa sera za fedha, mwenendo mzuri wa urari wa mapato ya fedha za kigeni, pamoja na usimamizi wa bajeti ya Serikali. Mapato ya kodi kwa mwaka 2017/18 yanatarajia kufikia asilimia 13.0 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 13.3 mwaka 2016/17. Aidha, nakisi ya bajeti inatarajia kufikia asilimia 2.1 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 1.5 mwaka 2016/17.

### 3.4.2 Uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Wizara imeandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/19. Mpango huu ni wa tatu katika kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21). Utekelezaji wa Mpango utasaidia Taifa kujenga msingi wa uchumi wa viwanda ili kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Hivyo, Serikali inaendelea kuandaa

mazingira wezeshi kwa ushiriki wa sekta binafsi katika kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Aidha, Wizara imekamilisha na kuchapisha Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2016/17-2020/21. Mkakati huo unatoa mwongozo wa kimkakati wa utekelezaji wa Mpango ambao utaiwezesha Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo 2025. Mkakati unalenga maeneo yafuatayo: viwanda vya nguo, ngozi, madawa, maeneo maalum ya kiuchumi na viwanda, ukuaji wa miji na usimamizi wa maendeleo ya miji.

**19.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Kitaifa ya Maendeleo iliyobainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta ilifanya ufuatiliaji wa miradi 29 katika mikoa ya Morogoro, Shinyanga, Mwanza, Pwani, Iringa na Mbeya. Miradi iliyofuatiliwa ilijumuisha miradi ya sekta ya Umma na Binafsi, katika sekta za Viwanda, Kilimo, Uvuvi, Maji, Afya, Elimu, Mifugo, Ujenzi na Miundombinu. Malengo makuu ya ufuatiliaji yalikuwa kubainisha hatua halisi za utekelezaji wa miradi husika, changamoto na hatua stahiki za

kuzitatua. Ufuatiliaji huo umekuwa msingi wa maandalizi ya Mpango wa mwaka 2018/19.

### 3.4.3 Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Wizara iliendelea kufuatilia jitihada za kupambana na umaskini nchini ambayo ni pamoja na kukamilisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini. Mfumo huu umebainisha viashiria vyote muhimu vya ufuatiliaji hali ya umaskini ikiwemo matokeo ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030. Aidha, viashiria hivi pia vimejumuishwa katika Mfumo mpya wa Kanzi Data (Local Government Monitoring Database) unaoratibiwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili kuweza kupata taarifa za jitihada za kupunguza umaskini katika ngazi ya Mamlaka ya Serikali za Mtaa kwa wakati. Viashiria hivyo ni pamoja na vile vinavyohusu masuala ya kilimo, mifugo, uvuvi, mazingira, elimu, afya, maji, kinga ya jamii, ajira na jinsia.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha Taarifa ya Hali ya Umaskini na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2016/17. Taarifa

hii inabainisha mwelekeo wa hali ya umaskini, changamoto na jinsi ya kukabiliana nazo. Aidha, inatupa viashiria vitakavyotumika na kubainisha wapi tulipoanzia (baselines) ili kupima mafanikio katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taarifa hiyo na hasa kwa kuzingatia tathmini ya viashiria vya umaskini usio wa kipato inaonesha mafanikio yafuatayo: wastani wa umri wa kuishi umeongezeka na kufikia miaka 64.3 mwaka 2017; vifo vya watoto wachanga vimepungua hadi kufikia watoto 36.4 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2016; kuongezeka kwa pato la wastani la mtanzania kutoka shilingi 1,918,931 mwaka 2015 na kufikia shilingi 2,131,299 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 11.1; kuongezeka kwa umiliki wa samani katika kaya; kuboreka kwa upatikanaji wa huduma za jamii ikiwemo elimu, afya ya jamii, maji safi na salama, umeme na miundombinu ya barabara.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini ya hali ya umaskini nchini iliyofanyika mwaka 2015/16 kwa ushirikiano baina ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Benki ya Dunia ilionesha kuwa umaskini wa mahitaji ya msingi umeendelea kupungua kutoka

asilimia 28.2 mwaka 2011/12 hadi asilimia 26.4 mwaka 2015/16. Malengo ya Serikali ni kupunguza umaskini hadi kufikia asilimia 12.7 mwaka 2025/26. Hata hivyo, ili kubainisha hali ya umaskini hususan wa kipato, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ikishirikiana na Benki ya Dunia hivi sasa inaendesha Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi (Household Budget Survey -HBS) kwa mwaka 2017/18. Hatua iliyofikiwa ni ukusanyaji wa takwimu za mapato na matumizi ya kaya kwa miezi sita ya kwanza ya 2018 katika mikoa yote. Kwa msingi huo tunatarajia kuwa matokeo rasmi ya hali halisi ya umaskini na hususan wa kipato katika ngazi ya kitaifa, kimkoa na kiwilaya yatatolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu mwezi Machi, 2019.

### 3.4.4 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

#### (a) Mapato ya Ndani

**24.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18, sera za mapato zililenga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya shilingi bilioni 19,997.0 ikijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi Aprili, 2018 jumla ya makusanyo ya

ndani ikijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalikuwa shilingi bilioni 14,838.5, sawa na asilimia 74 ya makadirio ya mwaka. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 12,661.0 sawa na asilimia 74 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi bilioni 17,106. 4; mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 1,789.9 sawa na asilimia 82 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi bilioni 2,183.4; na mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalikuwa shilingi bilioni 437.6, sawa na asilimia 64 ya makadirio ya shilingi bilioni 687.3 kwa mwaka.

**25.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili 2018, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 4,958.0 kutoka soko la ndani sawa na asilimia 80 ya shilingi bilioni 6,168.9 zilizotarajiwa kukopwa kwa mwaka. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 4,125.7 zilikopwa kwa ajili ya kulipia dhamana na hati fungani za Serikali zilizoiva (rollover), na shilingi bilioni 832.3 zilikopwa ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha, mikopo kutoka kwenye chanzo hiki, ilielekezwa kulipia sehemu ya madeni ya wakandarasi wa barabara na maji na umeme.

### (b) Misaada na Mikopo nafuu toka kwa Washirika wa Maendeleo

**26.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili 2018 Serikali imepokea kiasi cha shilingi bilioni 1,865.76 sawa na asilimia 47 ya lengo la shilingi bilioni 3,971.10. Kati ya kiasi kilichopokelewa, shilingi bilioni 70.2 ni Misaada na Mikopo nafuu ya Kibajeti (GBS) sawa na asilimia 7 ya ahadi ya shilingi bilioni 941.26, shilingi bilioni 180.52 ni za mifuko ya pamoja ya kisekta sawa na asilimia 33 ya ahadi ya shilingi bilioni 556.08 na shilingi bilioni 1,612.61 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 65 ya ahadi ya shilingi bilioni 2,473.77.

**27.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Sekta, Washirika wa Maendeleo, na Wadau wengine wa Maendeleo nchini ilifanikiwa kuandaa na kukamilisha Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo *(Development Cooperation Framework - DCF)* ambao uliidhinishwa na Serikali mwezi Agosti 2017. Mwongozo huu umeanza kutekelezwa mwaka 2017/18 na utadumu hadi 2024/25. Aidha, Wizara imeendelea kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo inayonufaika na rasilimali za nje ili kuhakikisha kwamba rasilimali zinatumika kwa mujibu wa

makubaliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo.

### 3.4.5 Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

**28.** ***Mheshimiwa Spika***, katika uandaaji na usimamizi wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/18, Wizara ilifanya Uboreshaji wa Mfumo wa Uandaaji na Usimamizi ya Bajeti ya Serikali (Central Budget Management System – CBMS) ambao umeanza kutumika rasmi katika uandaaji wa bajeti ya mwaka 2018/2019. Pamoja na mambo mengine, CBMS itarahisisha uandaaji na usimamizi wa bajeti ya Serikali ikiwa ni pamoja na utoaji na uchambuzi wa taarifa za mapato na matumizi na pia na utaondoa kabisa tatizo la uingizwaji wa takwimu za bajeti mara mbili kama ilivyokuwa kwenye mifumo iliyopita. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni: kuendesha mafunzo ya mfumo wa CBMS kwa maofisa 246 kutoka kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea na Sekretariati za Mikoa; kuandaa, kuweka kwenye tovuti ya wizara, kuchapisha na kusambaza nakala 3,000 za Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa mwaka 2018/19 kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na

Mamlaka za Serikali za Mitaa; ukamilishaji wa Vitabu vya Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2018/19 Juzuu Na. II, III na IV ambapo nakala 2,150 zilichapishwa na kuwasilishwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na pia kusambazwa kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea na Sekretarieti za Mikoa na Wadau wengine; na uandaaji wa Kijitabu cha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/18 Toleo za Wananchi (Citizens Budget) kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutumia fursa za kimapato zilizopo katika maeneo yao ili kutoa huduma bora na za uhakika kwa wananchi, katika mwaka 2017/18 Wizara imeanza kutekeleza mkakati wa kuziwezesha Serikali za Mitaa kujitegemea kimapato kupitia miradi ya kimkakati. Mkakati huu utaziwezesha Serikali za Mitaa zinazotekeleza miradi ya aina hiyo kujitegemea na hivyo kuiwezesha Serikali Kuu kuongeza nguvu na msukumo katika Halmashauri zenye uhitaji zaidi. Mkakati huu umeanza kutekelezwa katika baadhi ya Halmashauri zilizo katika mkoa wa Dar es Salaam baada ya kukidhi vigezo vilivyowekwa. Halmashauri hizo ni Ilala, Kinondoni, Ubungo na Jiji la Dar es Salaam. Aidha,

Halmashauri nyingine zote zimeelekezwa kuandaa Andiko la Miradi ya Kimkakati na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuchambuliwa na kuidhinishwa kwa kuzingatia vigezo.

### 3.4.6 Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali imeendelea kufanya uhakiki wa madeni ya Serikali kama ifuatavyo: Uhakiki wa madeni ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (NSSF, PPF, PSPF, GEPF, LAPF na NHIF), uhakiki wa madeni ya Mamlaka ya Uchimbaji Visima (DDCA) uliofanyika katika Halmashauri mbalimbali za mikoa ya Katavi, Morogoro, Arusha, Pwani na Lindi na kiasi cha shilingi bilioni 1,166.85 kiliokolewa kutokana na uhakiki huo; na uhakiki wa madeni ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali 61 na Sekretarieti za Mikoa 26 umekamilika; Aidha, Wizara imefanya ukaguzi maalum katika maeneo yafuatayo; Hospitali Teule ya Mvumi Dodoma; Mradi wa *SELF Microfinance Fund*, kuchunguza ukwepaji wa kodi katika Biashara ya vinywaji vikali; Kukagua mfumo wa kukusanya maduhuli

(ITS/AFCS system) wa Wakala wa Usafiri wa Mwendo wa Haraka (DART) na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA).

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu mengine yaliyotekelezwa ni pamoja na kusimamia na kuendeleza Kada ya Ukaguzi wa Ndani na Kamati za Ukaguzi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara iliendesha mafunzo mbalimbali kama ifuatavyo: mafunzo ya nadharia kwa wakaguzi 80; mafunzo kwa vitendo kwa wakaguzi 40; Mafunzo ya mwongozo wa Ukaguzi kwa Wakaguzi 82, na mafunzo ya uwekaji wa kumbukumbu za ukaguzi kwa wakaguzi 56 wa halmashauri 25; Mafunzo ya usimamizi wa Vihatarishi kwa Waratibu 57 na kwa wakuu wa Idara katika Wizara 15, Sekretariati za Mikoa 8 na Mamlaka za Serikari za Mitaa 15. Aidha, Wizara imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mwongozo wa Usimamizi wa Vihatarishi katika Sekretarieti za mikoa 2 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 17. Vile vile, uhakiki wa Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund) ulifanyika ambapo baada ya kukamilisha uhakiki huo, wahisani wa maendeleo waliweza kuchangia kiasi cha shilingi bilioni 450 kwenye bajeti ya Afya ya mwaka 2017/18.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea na jitihada za kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti ya Serikali, ili kuhakikisha kuwa thamani ya fedha inapatikana. Hadi kufikia Aprili, 2018 Wizara imefanya uhakiki na ufuatiliaji wa madai mbalimbali ya miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida yenye jumla ya shilingi 257,595,511,890.78 na Dola za Kimarekani 35,938,613.86 ambapo jumla ya shilingi 101,905,642,146.19 na Dola Kimarekani 10,034,161.82 zimeokolewa sawa na asilimia 40 ya madai yaliyoombwa kwa shilingi na asilimia 28 kwa madai ya Dola za Kimarekani. Miradi iliyohakikiwa ni pamoja na madai ya fidia kupisha upanuzi wa viwanja vya ndege, ujenzi wa chuo kikuu, madai ya Wakandarasi, madai ya marejesho ya Kodi na uhakiki wa miche ya korosho. Vile Vile, Wizara ilifanya ufuatiliaji wa matumizi ya shillingi bilioni 178.3 zilizotolewa kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kupitia MSD na uhakiki wa maombi ya fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa vituo vya afya.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia ulipaji wa mishahara ya watumishi wa Serikali na kuwezesha malipo kufanyika kwa watumishi wanaostahili tu, Wizara iliendelea kufanya uhakiki

wa taarifa za kiutumishi na mishahara katika taasisi za Serikali. Pia Wizara ilifanya uhakiki wa madai ya malimbikizo ya mishahara kwa watumishi 82,111 waliokuwa wanadai shilingi bilioni 127.61 ambapo madai halali yalikuwa shilingi bilioni 43.33 kwa watumishi 27,345 na hivyo kuokoa shilingi bilioni 84.28. Aidha, katika mwaka 2017/18 Wizara ilianzisha Mfumo mpya wa usimamizi na udhibiti wa mishahara ujulikanao kwa jina la *Government Salary Payment Platform-GSPP.* Mfumo huo unawawezesha waajiri kuhakiki taarifa za watumishi kwa urahisi na kuwaondoa watumishi wasiostahili kwa wakati kwenye orodha ya malipo ya mishahara.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa bajeti za Wizara; Idara Zinazojitegemea na Wakala; Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, wizara imeendelea kutoa fedha kwa Mafungu mbalimbali kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), Mishahara (PE), pamoja na Fedha za Maendeleo. Kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Aprili 2018 jumla ya shilingi trilioni 16.7 zimetolewa kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo na shilingi trilioni 4.9 zimetolewa kwa ajili ya Maendeleo.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto za madeni kwa Taasisi za Serikali, wizara imeandaa Mkakati wa Kulipa na Kuzuia Ulimbikizaji wa Madeni. Ili kuhakikisha mkakati huu unatekelezwa, Wizara tayari imeandaa Waraka wa HAZINA Na. 1 wa mwaka 2018/19 kuwataka Maafisa Masuuli wote wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia utekelezaji wa Waraka huo ili kuondokana na changamoto ya ulimbikizaji wa madeni.

**36.** ***Mheshimiwa Spika*****,** pamoja na mambo mengine, Waraka huo unawaagiza Maafisa Masuhuli kutekeleza yafuatayo: kutenga fedha za kutosha kwenye miradi ya maendeleo inayoendelea kabla ya kuanza miradi mipya; kufanya uhakiki wa madeni mapema kabla ya malipo; kutenga fedha za kulipa madeni kwenye bajeti zao; na kuhakikisha kuwa uagizwaji wa bidhaa unafanyika baada ya kutolewa kwa hati ya ununuzi (LPO) kwenye mfumo rasmi wa malipo (IFMS). Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuoanisha mifumo ya kutunza kumbukumbu za madeni ili kuwa na taarifa sahihi.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Serikali ilitenga shilingi bilioni 1,295 kwa ajili ya kulipa madeni ya Wazabuni, Wakandarasi, Watoa Huduma na Watumishi wa Umma baada ya kufanyiwa uhakiki. Hadi Aprili, 2018 jumla ya shilingi bilioni 1,167.7 zililipwa sawa na asilimia 90 ya lengo. Kati ya hizo, shilingi bilioni 81.8 zilikuwa ni kwa ajili ya madeni ya Wazabuni, shilingi bilioni 846.5 kwa ajili ya Wakandarasi, shilingi bilioni 78 kwa ajili ya Watoa huduma, shilingi bilioni 133.8 kwa ajili ya Watumishi na shilingi bilioni 27.6 kwa ajili ya madeni mengineyo.

### 3.4.7 Usimamizi wa Malipo

38. ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2017/18, Wizara imeendelea kuboresha usimamizi wa malipo kwa kuunganisha mfumo wa malipo wa TISS katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani, Kagera, Geita, Simiyu, Shinyanga, Mara, Kilimanjaro, Manyara, Singida, Tabora na Kigoma. Aidha, mfumo wa TISS umeunganishwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 25 na 37), Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (Fungu 57), Jeshi la Polisi (Fungu

28), Jeshi la Wananchi (Fungu 38), Jeshi la Kujenga Taifa (Fungu 39) na kuwapatia mafunzo Watumishi ili kuwawezesha kutumia mfumo huo. Vile vile, Wizara imesimika mfumo wa malipo (EPICOR) kwenye ubalozi wa Tanzania kule Nairobi-Kenya kwa lengo la kudhibiti matumizi nje ya bajeti. Kadhalika, Wizara imetoa mafunzo ya matumizi ya viwango vya kimataifa (IPSAS) kwenye uandaaji wa Hesabu kwa Wahasibu wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma 650 na kuwezesha kuandaa Hesabu za Majumuisho kwa mwaka wa fedha 2016/17 kwa kutumia Viwango vya Kimataifa (IPSAS Accrual Basis).

### 3.4.8 Deni la Serikali

**39.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kusimamia Deni la Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada SURA 134. Mwezi Novemba 2017, Serikali ilifanya tathmini ya uhimilivu wa Deni la Serikali kwa kipindi kilichoishia Juni 2017. Tathmini hiyo inaonesha kuwa deni ni himilivu kwa kipindi cha muda wa kati na muda mrefu. Uwiano wa Deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 34.4 ikilinganishwa na ukomo wa

asilimia 56; thamani ya sasa ya Deni la nje pekee kwa pato la Taifa ni asilimia 19.7 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 81.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 150; na thamani ya sasa ya deni la nje kwa mapato ya ndani ni asilimia 117.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 250. kazi ya viashiria hivi vinne nilivyovitaja ni kupima uwezo wa nchi kukopa.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kutokana pia na tathmini hiyo, ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani umefikia asilimia 9.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20 na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mauzo ya bidhaa nje ni asilimia 13.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20. Viashiria hivi vinapima uwezo wa nchi kulipa deni. Kwa kuzingatia vigezo hivi, Tanzania bado ina uwezo wa kuendelea kukopa kutoka ndani na nje ya nchi ili kugharamia shughuli zake za maendeleo na pia ina uwezo wa kulipa mikopo inayoiva kwa kutumia mapato yake ya ndani na nje kwa wakati.

**41.** ***Mheshimiwa Spika***, Pamoja na uhimilivu huo Serikali imeendelea kuchukua tahadhari kwa kukopa kwenye vyanzo vyenye masharti na gharama nafuu na kuhakikisha kuwa mikopo hiyo

inaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo yenye vichocheo vya ukuaji wa uchumi ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege na ujenzi wa mitambo ya kufua Umeme. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kila robo mwaka inapitia viwango vya Deni la Serikali ili kuhakikisha kuwa deni linaendelea kuwa himilivu. Vile vile, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekamilisha ukaguzi wa deni hilo na Serikali inapitia taarifa hiyo kwa lengo la kuzingatia ushauri uliotolewa.

**42.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 1,262.42 kwa ajili ya kulipa riba ya deni la ndani ambapo hadi kufikia Aprili, 2018 kiasi cha shilingi bilioni 1,099.57 kimelipwa sawa na asilimia 87.10 ya lengo. Aidha, Serikali ilitenga shilingi bilioni 685.06 kwa ajili ya kulipa riba ya deni la nje. Hadi Aprili 2018 shilingi bilioni 528.17 zimelipwa sawa na asilimia 77.10 ya lengo.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Serikali ilitarajia kukopa kutoka soko la ndani kiasi cha shilingi bilioni 4,835.19 kwa ajili ya kulipia mtaji (rollover) wa deni la ndani. Hadi kufikia Aprili 2018 kiasi cha shilingi bilioni 4,125.65 kilikopwa

kutoka soko la ndani kwa ajili ya kulipia mtaji wa deni la ndani sawa na asilimia 85.33 ya lengo. Aidha, Serikali ilitenga shilingi bilioni 1,319.13 kwa ajili ya kulipia mtaji wa deni la nje ambapo hadi kufikia April, 2018 shilingi bilioni 1,118.29 zimelipwa sawa na asilimia 85 ya lengo.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** kulipa deni la ndani na nje kwa ukamilifu na kwa wakati husaidia kuiweka nchi katika nafasi nzuri ya kukopesheka zaidi kwa kuwa wakopeshaji hutegemea taarifa ya tathmini ya nchi kukopesheka na ulipaji wa deni kwa ukamilifu na kwa wakati ni sehemu muhimu ya tathmini hiyo.

### 3.4.9 Usimamizi wa Mifumo ya Taarifa za Kifedha

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea na kazi ya kuboresha Mfumo wa kutolea taarifa za kulipia mishahara kwa watumishi wa Umma kwa njia ya Kielektroniki (*Government Salaries Payment Platform and Government Online Salary Slip Portal*) ambapo mfumo wa kutolea taarifa za malipo ya Mishahara ya watumishi wa Umma na hati za mishahara (*Government Salary Slip Portal*) ulikamilika na

kuanza kutumika mwezi Julai, 2017. Watumishi wa umma wanaweza kupata hati za mishahara kwa njia ya kielektroniki mahala popote palipo na mtandao. Aidha, maboresho haya yamepunguza gharama kubwa za usambazaji wa taarifa za mishahara. Pia Wizara imesimika mfumo wa makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi, (Government electronic Payment Gateway - GePG) ambapo hadi sasa taasisi 86 zimeunganishwa na kati ya hizo taasisi 51 zimeanza kukusanya maduhuli kwa njia ya kielektroniki.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na kazi ya kuunganisha mifumo ya kielektroniki ya taarifa za kifedha ambapo mifumo mbalimbali ya kifedha imeunganishwa. Mifumo ambayo imeunganishwa na inabadilishana taarifa ni Mfumo wa Malipo ya Mishahara ya Watumishi wa Serikali (*Government Salaries Payment Platform - GSPP*); Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (*Human Capital Management Information - HCMIS);* na Mfumo wa Malipo wa Serikali (IFMS). Aidha, mifumo mingine iliyounganishwa katika mfumo wa pamoja wa kubadilishana taarifa (*Ministry of Finance Electronic Service Bus - MoF ESB)* ni Mfumo wa Malipo wa *Government Payment Platform* - GPP, Mfumo wa Malipo ya

Mishahara ya Watumishi wa Serikali (GSPP), Mfumo wa Malipo wa Kielektroniki (EFT & TISS), Mfumo wa Malipo wa Benki Kuu (CBS), mfumo wa malipo ya Pensheni (*Pension Payroll)* na Mfumo wa malipo ya Bunge (*Bunge Payroll*).

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** uunganishwaji wa mifumo hii umeleta mafanikio serikalini kwani mishahara ya watumishi wa serikali inalipwa moja kwa moja kupitia Benki Kuu ya Tanzania bila kutumia mawakala kama ilivyo kuwa zamani. Aidha, wizara ilitengeneza Mfumo wa Maombi ya Ulipaji wa Vibali vya Wageni Kufanya Kazi Ndani ya Nchi (*Work Permit System*) kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana Ajira, na Watu wenye Ulemavu.

### 3.4.10 Usimamizi wa Mali za Serikali

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora wa Mali za Serikali, Wizara imeendelea kufanya uthamini wa mali katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali. Hadi Aprili 2018, uthamini wa ardhi na majengo ya Serikali katika Mafungu 48 ulifanyika ili kuwa na taarifa sahihi za mali za Serikali za Mafungu hayo. Aidha, Wizara imefanya uhakiki maalum wa Mali za Watu

binafsi zilizo chini ya uangalizi wa Serikali kwa vituo 145 vya Polisi Tanzania Bara na Zanzibar kwa lengo la kuipunguzia Serikali mzigo wa kulipa fidia zinazotokana na upungufu wa uangalizi na usimamizi wa Mali hizo.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na zoezi la uondoshaji wa mali chakavu katika Wizara, Taasisi, Wakala, Mikoa, Idara zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.26 zilikusanywa kutokana na mauzo ya mali hizo. Aidha, Wizara imekusanya kiasi cha shilingi milioni 180.23 ikiwa ni fidia kutoka kampuni za Bima kutokana na ajali zilizosababisha uharibifu wa magari ya Serikali na tozo kwa Watumishi wa Umma kutokana na upotevu wa Mali za Serikali. Vile vile Wizara imelipa fidia na kifuta machozi ambapo jumla ya shilingi milioni 164.74 zimelipwa kutokana na amri za Mahakama.

### 3.4.11 Ununuzi wa Umma

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Wizara imetoa mafunzo kwa maafisa ununuzi na ugavi 75 juu ya matumizi ya mfumo wa uagizaji wa mahitaji wa Hati ya Ununuzi (*Local Purchase*

*Order-LPO*) kupitia Mfumo wa Malipo ya Serikali (Epicor); na kukamilisha zoezi la tathmini ya Ufanisi wa Mfumo wa Ununuzi wa Umma na kuandaa mikakati ya utekelezaji wa matokeo ya zoezi hilo.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imekamilisha utayarishaji wa mfumo wa ununuzi kwa njia ya mtandao (Tanzania National e-Procurement System – TANePS). Mfumo huo ulisimikwa tarehe 27 Februari 2018, na unapatikana kwenye anwani mtandao ya www.taneps.go.tz. Kupitia mfumo huu, kampuni zimeanza kujisajili, hatua itakayoziwezesha kushiriki katika ununuzi kwa njia ya mtandao. Mafunzo ya matumizi ya mfumo kwa wadau mbalimbali, ikiwemo taasisi nunuzi 100 za majaribio na wafanyabiashara yanaendelea na majaribio yataanza mwaka wa fedha wa 2018/19 kwa ununuzi wa bidhaa mtambuka, madawa na bidhaa tiba. Aidha, Mamlaka imetengeneza miongozo mbalimbali ya ununuzi wa Umma ikiwemo: kuwezesha ushiriki wa makundi maalum kwenye ununuzi; ushiriki wa taasisi za umma kwenye ununuzi; ununuzi wa vifaa, malighafi, bidhaa na huduma kwa maendeleo ya viwanda;

kupima tofauti kubwa na ndogo kwenye ununuzi wa umma; na kukodi kumbi kwenye taasisi za umma. Aidha, mafunzo maalum ya Sheria, Kanuni na Miongozo ya Ununuzi wa Umma yametolewa kwa watumishi 522 kutoka Taasisi mbalimbali za umma.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imefanya ukaguzi wa ununuzi wa umma wa mwaka 2016/17 katika taasisi nunuzi 112. Matokeo ya ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria kwa taasisi hizi ulikuwa ni wa asilimia 74 wakati matokeo ya ukaguzi wa kupima thamani halisi ya fedha kwa taasisi zilizokaguliwa ulikuwa ni asilimia 82.5. Ukaguzi huu ulibaini uwepo wa viashiria vya rushwa kwenye taasisi 17 zenye miradi 34, ambapo matokeo hayo yaliwasilishwa TAKUKURU kwa hatua zaidi.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2018, Wizara kupitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: kununua magari 398 kwa gharama ya shilingi bilioni 51.52 kupitia utaratibu wa ununuzi wa magari ya Serikali kwa pamoja ambapo Serikali imeweza kuokoa shilingi bilioni 3.45; kutoa

mikataba 8,346 kwa wazabuni na watoa huduma ambao watatoa huduma mbalimbali kwa taasisi za umma kupitia utaratibu wa ununuzi kwa mikataba maalum; kutekeleza mradi wa usimamizi na udhibiti wa mafuta kwenye magari ya Serikali katika mikoa saba (7) ya Arusha, Dodoma, Morogoro, Mwanza, Mtwara, Ruvuma na Singida; na kusimika matanki yenye ujazo wa lita 30,000 katika mikoa ya Kigoma na Iringa ili kuongeza uwezo wa kuhifadhi mafuta.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma ilipokea jumla ya rufaa 36 sawa na asilimia 120 ya lengo la kupokea rufaa 30. Kati ya hizo, rufaa 34 zilitolewa maamuzi sawa na asilimia 94 ya rufaa zilizopokelewa. Kati ya rufaa zilizotolewa maamuzi, taasisi nunuzi zilishinda rufaa 17 na wakata rufaa walishinda rufaa 14. Rufaa mbili ziliondolewa na waomba rufaa wenyewe na rufaa moja ilirudishwa kwa mujibu wa sheria. Aidha, rufaa mbili (2) zipo kwenye hatua za awali za kusikilizwa.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2018 Wizara kupitia Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi ilitekeleza yafuatayo: Kuendesha kongamano la mwaka 2017 la wataalam wa Ununuzi na Ugavi

lililo shirikisha jumla ya wataalam 600 kutoka ndani na nje ya nchi; Kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya kujenga uwezo na ufanisi wa wanataaluma kwa wastani wataalam 50 kwa mwezi; Kusajili wanataaluma wapya 1,854 katika ngazi mbalimbali na Kuendesha mitihani ya kitaaluma katika ununuzi na ugavi ambapo watahiniwa 1,519 walitahiniwa katika mitihani iliyofanyika mwezi Novemba, 2017.

### 3.4.12 Ukaguzi wa Hesabu za Serikali

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17. Ofisi ilifanya ukaguzi wa hesabu za Wizara na Idara za Serikali zinazojitegemea 55, mikoa yote 26 ya Tanzania Bara; Wakala za Serikali 37, Mifuko maalum 15, Taasisi nyingine za Serikali 60, Balozi za Tanzania nje ya nchi 40. Aidha, ukaguzi ulifanyika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 na Mashirika ya Umma 105.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa upande wa miradi ya maendeleo, jumla ya ripoti 742 za ukaguzi zimetolewa. Aidha, katika ukaguzi wa ufanisi, jumla ya ripoti 10 zimetolewa katika kipindi kilichoishia Aprili, 2018. Hadi kufikia Aprili, 2018 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iliweza kutoa Ripoti kuu 5. Ripoti hizo ni muhtasari wa jumla ya ripoti 1,269 zilizotolewa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17. Ofisi imewezesha ripoti hizo kuwasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu, tarehe 27 Machi, 2018 kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, Ofisi imefanikiwa kufanya ukaguzi maalum wa Idara ya Uhamiaji, Soko la Mwanjelwa, Chama cha Waalimu Tanzania (CWT), Jumuiya ya Serikali za Mitaa Tanzania - ALAT, Shirika la Utangazaji la Taifa - TBC, NIDA na Ubia kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) na Kampuni ya Intra Energy Tanzania Limited (IETL).

### 3.4.13 Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18 Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imefanya tathmini na uchambuzi wa Mikataba ya Utendaji Kazi 31 iliyoingiwa baina ya Msajili wa Hazina na Wenyeviti wa Bodi za Taasisi na Mashirika ya

Umma katika mwaka 2016/17. Lengo la zoezi hilo ni kupima utekelezaji wa mikataba hiyo kwa mujibu wa viashiria vya mafanikio ambapo mambo ya msingi yanayozingatiwa katika tathmini ni: utawala bora; usimamizi wa fedha; usimamizi wa rasilimali watu; na huduma kwa mteja. Katika zoezi la Mikataba ya Utendaji, kigezo ni taasisi husika kuwa na bodi hai na kuwa na bajeti iliyoidhinishwa. Matokeo ya tathmini yanaonesha wastani wa taasisi kufanya vizuri kwa asilimia 70.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kufanya uchambuzi wa taasisi na mashirika ya umma ambayo majukumu yao kwa namna moja au nyingine yanafanana kwa lengo la kuunganisha taasisi hizo ili kuongezea tija na kupunguza gharama za uendeshaji.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Msajili wa Hazina imekamilisha Taarifa ya Uwekezaji wa Serikali kwenye Mashirika na Taasisi za Umma kwa mwaka 2016/17 na kuiwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Sheria. Taarifa hii inabainisha uwekezaji; mikopo na dhamana zilizotolewa na Serikali kwa taasisi; na makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi kutoka katika taasisi hizo. Taarifa hiyo imebainisha

kuwa uwekezaji wa Serikali katika taasisi za umma umefikia shilingi trilioni 48.5.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya tathmini na ufuatiliaji kwenye viwanda 85 na mashamba 12 yaliyobinafsishwa kwa lengo la kukagua ufanisi na kuhakiki utekelezaji wa masharti ya mikataba ya mauzo. Katika zoezi hilo, jumla ya viwanda 10 vilibainika kukiuka Masharti ya Mikataba ya Mauzo na wawekezaji wake kutoonesha nia ya dhati ya kuviendeleza viwanda hivyo. Kwa sasa Serikali iko katika hatua za urejeshaji wa viwanda hivyo kwa kuzingatia Sheria na taratibu za nchi.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2018, Wizara imefanya kaguzi za kimenejimenti katika taasisi nane (8) ambazo ni *Marine Parks Service Unit*, Baraza la Ujenzi la Taifa, Tume ya UNESCO, Baraza La Taifa la Kiswahili, Mamlaka ya Biashara (TANTRADE), Benki ya TPB, Shirika la Masoko Kariakoo na Bodi ya Pareto. Kaguzi hizo zimebaini kuwa: mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Hoja zinazotolewa na Mkaguzi wa Ndani kutokutekelezwa kikamilifu; matumizi yasiyoridhisha ya rasilimali watu na fedha; na kuwepo kwa madeni ya wazabuni ya

muda mrefu yaliyolimbikizwa. Aidha, hatua mbalimbali zimechukuliwa ili kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa katika kaguzi hizo ikiwemo: kuzijulisha Wizara Mama, Bodi za taasisi, pamoja na mamlaka nyingine za Serikali matokeo ya kaguzi ili ziweze kuchukua hatua stahiki; na kuziagiza taasisi husika kuandaa miongozo inayohitajika katika uendeshaji wa taasisi na mashirika.

### 3.4.14 Mafao ya Wastaafu na Mirathi

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 1,008.61 kwa ajili ya kulipia michango ya mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hadi kufikia Aprili, 2018 kiasi cha shilingi bilioni 716.19 sawa na asilimia 71 kilitumika kulipa michango ya mwajiri kwa watumishi wa umma. Aidha, ninatumia fursa hii kuiagiza Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iandikishe wanachama wake, kuwapa vitambulisho vya uanachama na kutunza vizuri na kwa usahihi taarifa za uchangiaji kwa kipindi chote cha utumishi wa wanachama ili kuwaondolea usumbufu siku za kustaafu kwao kama ilivyoelekezwa na Miongozo ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Vile vile, nawaomba

watumishi wa Umma wawe na tabia ya kukagua taarifa za madaraja ya mishahara, makato ya lazima na yale yasiyo ya lazima kutoka kwenye mishahara yao na kutoa taarifa kwa wakati kwa mamlaka husika ili kama kuna makato hayako sawasawa mamlaka husika zichukue hatua za kurekebisha mapema na kuisaidia Serikali kuepuka tozo zinazoweza kutozwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi nyingine za fedha.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 421.89 kwa ajili ya kulipa mafao ya wastaafu na mirathi kwa wastaafu wanaolipwa mafao na Hazina. Hadi Aprili, 2018 kiasi cha shilingi bilioni 343.43 sawa na asilimia 81.40 kilitumika kulipia mafao ya wastaafu 4,614, mirathi 1,301 na pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu 56,825. Aidha, katika juhudi za kurahisisha upatikanaji wa taarifa za wastaafu, kumbukumbu za wastaafu zimeendelea kuhifadhiwa kwenye mfumo wa TEHAMA unaoitwa SAPERION ambapo hadi Aprili, 2018 kumbukumbu za wastaafu 93,784 zimewekwa kwenye mfumo huo. Vile vile, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya malipo kwa wastaafu ambao wanalipwa na Hazina kwa kulipa pensheni ya kila mwezi na mirathi moja kwa moja kwenye akaunti

zao kwa kutumia mfumo wa TEHAMA wa Benki Kuu ya Tanzania.

### 3.4.15 Udhibiti wa Utakasishaji Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi

**65.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu kwa kufanya yafuatayo: Kupokea na kuchambua taarifa 254 za miamala shuku inayohusu fedha haramu na ufadhili wa ugaidi na kuwasilisha taarifa za kiintelijensia 32 kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kwa ajili ya uchunguzi. Aidha, Wizara katika kujenga uwezo wa watumishi, Maafisa wa Kitengo walipata mafunzo ya namna bora ya uchambuzi na upembuzi wa taarifa za miamala shuku katika Kituo cha Kudhibiti Fedha Haramu (Financial Intelligence Centre – FIC) cha Afrika ya Kusini na Maafisa wanne (4) walihudhuria mafunzo ya Financial Action Task Force (FATF) standards yaliyofanyika nchini Korea Kusini ambayo ni muhimu katika nyanja ya udhibiti wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

66. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara iliendelea kutoa elimu kwa wadau jinsi ya kutumia mfumo wa kompyuta wa goAML namna ya kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku kwa njia ya kielektroniki na uchambuzi . Vile vile, Wizara iliendesha mafunzo ya namna ya kutekeleza Kanuni za kutoa taarifa za usafirishaji na uingizaji wa fedha taslimu kutoka na kwenda nje ya nchi kwa Maafisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Kanuni hizo tayari zimeshaanza kutekelezwa tangu mwezi Oktoba 2017. Hadi Aprili, 2018 kitengo kimepokea jumla ya taarifa 2,790 za usafirishaji wa fedha taslimu toka mipaka yote ya Tanzania. Kadhalika, Kitengo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kimejenga uwezo wa kupambana na utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi kupitia mafunzo na mikutano ya pamoja na vyombo vya kusimamia utekelezaji wa sheria na Mamlaka za usimamizi ikiwemo, Jeshi la Polisi, Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar, Bodi ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi.

### 3.4.16 Tume ya Pamoja ya Fedha

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia Tume ya Pamoja ya Fedha imekamilisha Utafiti kuhusu Mfumo Bora wa Uwekezaji katika Mashirika na Kampuni zinazotekeleza Mambo ya Muungano. Utafiti umeonesha kuwepo kwa Mashirika na Kampuni tisa (9) yanayotekeleza Mambo ya Muungano, ambayo ni: Benki Kuu ya Tanzania; Shirika la Bandari Tanzania; Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania; Shirika la Posta Tanzania; Kampuni ya Simu Tanzania; Kampuni ya Ndege Tanzania; Benki ya Posta; Benki ya NMB; na Benki ya Biashara (NBC (1997) Ltd).

### 3.4.17 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Wizara imeendelea kuratibu na kuchambua miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na kuishauri Serikali juu ya utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha, kulingana na Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Sura 103; uchambuzi wa miradi ya Ubia hupitia hatua tatu zifuatazo; (i) Mamlaka za utekelezaji kuwasilisha andiko la awali

la mradi kwa ajili ya uchambuzi (ii) Mamlaka kuandaa taarifa ya awali ya upembuzi yakinifu (iii) Mamlaka ya utelekezaji wa miradi ikishirikiana na Mshauri Elekezi kuandaa na kuwasilisha Taarifa ya Upembuzi Yakinifu. Wizara hufanya uchambuzi wa taarifa hizo kwa kuangalia, pamoja na mambo mengine maeneo makuu matatu; (a) Uhamishaji wa mianya hasi ya mradi kwenda kwa sekta binafsi (b) Uwezo wa Serikali kugharimia mradi na (c) Manufaa ya mradi kwa Serikali na wananchi kwa ujumla. Endapo mradi unakidhi vigezo utaidhinishwa na Kamati ya Wataalam wa PPP kwa ajili ya kuendelea na hatua ya kumpata mbia.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefikia hatua mbalimbali za uchambuzi wa miradi itakayotekelezwa kwa utaratibu wa PPP. Upembuzi Yakinifu wa Mradi wa Uzalishaji wa Madawa muhimu na Vifaa Tiba wa Bohari Kuu ya Madawa (MSD) umekamilishwa na kuwasilishwa kwenye Kitengo cha Ubia kwa ajili ya hatua za uidhinishaji; Mradi wa Kujenga na Kuendesha Vyuo 10 vya VETA kwa Utaratibu wa PPP katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Manyara, Tabora na Shinyanga. Wizara imefanya uchambuzi wa Taarifa ya Upembuzi Yakinifu na kuwasilisha kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

mapendekezo yanayotakiwa kuzingatiwa ili mradi uwe na tija kwa Taifa; Mradi wa Barabara ya Tozo kutoka Dar Es Salaam hadi Chalinze, taarifa ya upembuzi yakinifu wa mradi imefanyiwa uchambuzi ambapo Wizara imetoa idhini yenye masharti *(Conditional Approval)* ya kutekeleza kabla ya kuendelea na hatua ya kumpata mbia; Mradi wa Uendeshaji wa Huduma ya Usafiri jijini Dar es Salaam Awamu ya kwanza, zabuni kwa ajili ya ununuzi wa mtoa huduma wa kudumu, mkusanyaji mapato na mwendesha mfuko zilitangazwa na wazabuni wamepatikana; na Wizara imekamilisha uchambuzi wa andiko la awali la mradi wa Mradi wa Mwambani Port lililowasilishwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania, hatua inayoendelea ni maandalizi ya Upembuzi Yakinifu.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kusimamia utekelezaji wa Programu ya PPP ili Mamlaka za Serikali zitumie utaratibu wa PPP katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/17-2020/21. Kutokana na jitihada hizi, maandiko ya miradi yanayoandaliwa ni pamoja na ujenzi wa Reli ya Mchuchuma/Liganga – Mtwara kwa kiwango cha *standard gauge* na ujenzi wa Reli ya Tanga – Arusha-Musoma kwa kiwango cha

*standard gauge;* ujenzi wa Miundombinu ya Reli katika Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya Treni ya abiria na mradi wa kusambaza Gesi asilia Nchini kwa kuanzia Jijini Dar es Salaam. Aidha, Wizara ipo Katika hatua za kukamilisha marekebisho ya Sheria ya PPP Sura 103 ili kuimarisha mfumo wa usimamiaji wa miradi ya PPP ikiwa ni pamoja na kupunguza mlolongo wa uidhinishaji miradi kupitia Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi nchini. Waraka huu upo kwenye hatua ya kujadiliwa na Baraza la Mawaziri.

### 3.5 USIMAMIZI NA URATIBU WA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA CHINI YA WIZARA

**71.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba sasa nieleze utekelezaji wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya Wizara kwa mwaka 2017/18 kama ifuatavyo:-

#### 3.5.1 HUDUMA ZA KIBENKI

#### (i) Benki Kuu ya Tanzania

**72.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Benki Kuu ya Tanzania ilifanya utafiti wa upatikanaji wa huduma za kifedha nchini (FinScope Survey)

mwaka 2017 kwa kushirikisha wadau mbalimbali kutoka katika sekta ya umma na sekta binafsi. Kwa ujumla matokeo ya utafiti huo yameonesha kwamba Tanzania imepiga hatua katika kusogeza huduma za kifedha karibu na wananchi. Hadi sasa asilimia 86 ya Watanzania wako umbali usiozidi kilometa 5 kutoka kituo cha huduma za kifedha, ambapo mijini ni asilimia 91 na vijijini ni asilimia 78. Aidha, Watanzania wanaotumia huduma za fedha wameongezeka na kufikia asilimia 65 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 57 ya mwaka 2013.

**73.** ***Mheshimiwa Spika***, Hadi Desemba 2017, utafiti wa upatikanaji wa huduma za kifedha nchini (FinScope Survey) umebaini wastani wa asilimia 65 ya Watanzania walikuwa wanatumia huduma rasmi za kifedha, asilimia 7 wanatumia huduma zisizo rasmi na asilimia 28 hawatumii kabisa huduma za kifedha. Kwa kuliona hili, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na washirika wa maendeleo imeandaa mpango mpya wa huduma jumuishi unaoweka msisitizo wa kuhakikisha kwamba asilimia 75 ya Watanzania wanatumia huduma rasmi za kifedha ifikapo mwaka 2022. Aidha, utafiti wa FinScope 2017 ulionesha kuwa asilimia 44 ya Watanzania wanakopa, na asilimia 10 ya wakopaji wote hukopa kwa ajili ya shughuli za kibiashara

wakati asilimia 8 hukopa kwa ajili ya shughuli za kilimo.

**74.** ***Mheshimiwa Spika***, Benki Kuu ilishusha riba yake (discount rate) kutoka asilimia 12 mwezi Machi 2017 na kufikia asilimia 9 mwezi Agosti 2017. Hatua hii pamoja na hatua nyingine zilizochukuliwa zilisaidia kuongeza ukwasi kwenye benki za biashara na kushusha riba katika masoko ya fedha. Riba ya siku moja katika soko la fedha baina ya mabenki (overnight interbank cash market rate) ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 1.2 mwezi Aprili 2018 kutoka asilimia 4.08 mwezi Juni 2017. Katika kipindi hicho, riba za dhamana za Serikali zilipungua hadi kufikia wastani wa asilimia 4.04 mwezi Aprili 2018 kutoka asilimia 7.64 mwezi Juni 2017. Aidha, riba za mikopo inayotolewa na benki za biashara zilipungua kidogo na kufikia wastani wa asilimia 17.51 kwa mwezi Machi 2018 kutoka asilimia 17.61 kwa mwezi Juni 2017 kutokana na benki hizo kuweka tahadhari kubwa kwa wateja wanaoshindwa kurejesha mikopo yao kwa wakati (risk premium), hali iliyochangiwa zaidi na kuongezeka kwa mikopo chechefu.

**75.** ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu ili kuongeza ukwasi kwenye uchumi, ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3), uliongezeka na kufikia asilimia 8.3 mwezi Machi 2018 kutoka asilimia 6.0 kwa mwaka ulioishia Juni 2017. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulipungua kwa wastani wa asilimia 1.5 katika kipindi kinachoishia Oktoba 2017 na ulianza kuimarika na kufikia asilimia 1.1 mwezi Machi 2018. Ukuaji huu bado ni mdogo ukilinganishwa na ukuaji wa tarakimu mbili uliofikiwa mara ya mwisho mwezi Oktoba 2016, sababu kubwa ikiwa ni tahadhari iliyochukuliwa na benki za biashara katika kutoa mikopo kufuatia ongezeko la mikopo chechefu pamoja na benki hizo kupendelea zaidi kuwekeza kwenye dhamana za Serikali.

**76.** ***Mheshimiwa Spika***, akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha na yenye kukidhi kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi ikiwa ni pamoja na kuongezeka imani kwa wawekezaji katika uchumi wetu. Akiba ya fedha za kigeni iliongezeka na kufikia Dola ya Marekani milioni 5,251.1 mwishoni mwa mwezi Aprili 2018, kutoka Dola ya Marekani milioni 5,000.4 mwishoni mwa mwezi Juni 2017. Akiba hii inatosha kulipia na

kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 5.4. Aidha, kufuatia kuimarika kwa urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho mali nchi za nje, thamani ya shilingi ya Tanzania imeendelea kuwa tulivu. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2017 hadi Aprili 2018 dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,241 na 2,275 ikilinganishwa na shilingi 2,181 hadi 2,254 katika kipindi cha Julai 2016 hadi Aprili 2017.

**77.** ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Desemba 2017, Benki Kuu ilitoa leseni kwa benki moja ya biashara (Guaranty Trust Bank (Tanzania) Ltd) na kuzifutia leseni benki tano (Efatha Bank Ltd, Covenant Bank for Women Tanzania Ltd, Njombe Community Bank Ltd, Kagera Farmers' Cooperative Bank Ltd na Meru Community Bank Ltd) na kuziweka chini ya ufilisi. Uamuzi huu ulichukuliwa baada ya Benki Kuu kujiridhisha kuwa benki hizo zilikuwa na upungufu mkubwa wa mtaji kinyume na matakwa ya sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na kanuni zake. Upungufu huo wa mtaji ulionekana kuhatarisha usalama wa sekta ya fedha na kwamba kuendelea kutoa huduma za kibenki kwa benki hizo kungeweza kuhatarisha usalama wa amana za wateja wake.

### (ii) Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB)

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2018, TADB imeidhinisha mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 56.1 na kufanya jumla ya mikopo iliyoidhinishwa kufika shilingi bilioni 87.1 tangu Benki kuanza rasmi shughuli za utoaji wa mikopo mwaka 2016. Mikopo hii imewanufaisha wakulima wa mazao ya mahindi, mpunga, miwa, korosho, pamba, karafuu pamoja na wafugaji wa ng'ombe wa maziwa na wafugaji wa samaki. Kiasi cha shilingi bilioni 10.81 ya mikopo iliyotolewa zilikuwa ni kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo kwa wakulima wa mahindi, mpunga, pamba na ufugaji wa samaki na shilingi bilioni 17.86 zilikuwa ni kwa ajili ya ununuzi wa mazao ya wakulima wa korosho na karafuu katika mikoa ya Kusini pamoja na Zanzibar.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Januari 2017 hadi Aprili, 2018, TADB imefanikiwa kutoa mafunzo kwa wakulima wadogo wadogo, wafugaji na wavuvi 4,905 katika mikoa mbalimbali nchini. Mafunzo haya yalilenga kuwajengea wakulima uwezo katika maswala ya usimamizi wa fedha, oganaizesheni ya vikundi na vyama,

utunzaji wa kumbukumbu na utengenezaji wa miradi inayokidhi masharti ya mikopo kutoka katika mabenki na taasisi za fedha.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** TADB imezindua miradi miwili mikubwa ya kilimo kwa ajili ya kuchochea uwekezaji katika sekta ya kilimo. Miradi hii ni Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima wadogowadogo na Mfuko wa Kuwezesha Ubunifu Vijijini iliyopo chini ya Programu ya *Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Finance Support Programme (MIVARF)* inayoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogowadogo unalenga kuchagiza mabenki ya biashara kuongeza utoaji wa mikopo kwa wakulima wadogowadogo nchini kwa kufidia hadi asilimia 50 ya mikopo itakayoshindikana kurejeshwa. Kwa upande mwingine, Mfuko wa Kuwezesha Ubunifu Vijijini utajikita katika kuchagiza na kufadhili mipango inayolenga kutumia ubunifu na mbinu mpya katika kuchochea maendeleo na kuongeza huduma za fedha vijijini.

### (iii) Benki ya Maendeleo TIB (TIB DFI)

**81.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Benki ya Maendeleo Tanzania ya TIB imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kutoa mikopo katika sekta za kimaendeleo. Hadi Aprili, 2018 benki ilikuwa imetoa mikopo inayofikia shilingi bilioni 549.07 ikilinganishwa na shilingi bilioni 641.85 mwezi Desemba, 2016. Upungufu huu unatokana na mkakati wa benki kuwekeza katika miradi yenye tija na faida zaidi hapo baadaye. Aidha, katika kutimiza azma ya uwekezaji katika mwaka 2018 benki imewekeza kiasi cha shilingi milioni 500 kama mtaji kwenye kampuni ya masoko ya mazao ya kilimo (Tanzania Mercantile Company) ambayo itawezesha kuondoa madalali kwenye mazao ya kilimo na kumpa faida mkulima wa kawaida.

### (iv) Benki ya TIB Corporate (TIB CBL)

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hadi Aprili, 2018, TIB CBL imeweza: Kutoa mikopo ya maendeleo katika sekta mbalimbali kufikia kiasi cha shillingi bilioni 156.12; kuidhinisha Dhamana za kibenki ("Bank Guarantee") zenye thamani ya shilingi bilioni 55.70; kuidhinisha mkopo wa muda mfupi

("overdraft") na Dhamana ya Malipo inayofikia shilingi bilioni 12.20; Kuidhinisha mkopo wa muda mfupi na Barua za Dhamana ("Letters of Credit") wenye thamani ya shilingi bilioni 20; na Utoaji wa mikopo ya muda mfupi ya kiasi cha shilingi bilioni 6. Aidha, hadi kufikia Aprili 2018, amana za wateja ziliongezeka na kufikia shilingi bilioni 258.64 kutoka shilingi bilioni 186.20 mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia 39.

### (v) Benki ya TPB

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017 Benki ya TPB imefanikiwa:- kuanzisha matawi madogo matano (5) wilayani na pembezoni mwa miji mikubwa; kufungua akaunti 51,004 na kufanya jumla ya akaunti kuwa 349,878; Aidha, amana za wateja (deposits) ziliongezeka na kufikia shilingi milioni 317,645, kutoka shilingi milioni 292,200 (kama Desemba 31,2016) sawa na ongezeko la asilimia 9. Dhamana za Serikali ziliongezeka na kufikia thamani ya shilingi milioni 61,764 - kutoka kiasi cha shilingi milioni 42,452 zilizowekezwa hadi Desemba 31, 2016 sawa na ongezeko la asilimia 45.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Desemba 2017, thamani ya mikopo ilikuwa shilingi bilioni 336.80 kutoka shilingi bilioni 298.06 Desemba 2016 sawa na ongezeko la asilimia 13. Aidha, Benki ilizalisha pato ghafi la jumla ya shilingi bilioni 107.96 ikilinganishwa na shilingi bilioni 81.71 mwaka 2016.

### 3.5.2 Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

#### (i) Mfuko wa Pensheni wa PSPF

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2017 hadi Aprili, 2018, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma umesajili jumla ya wanachama 5,228. Aidha, katika kipindi hicho Mfuko umekusanya shilingi bilioni 712.10 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali. Kiasi hicho kinajumuisha shilingi bilioni 571 ikiwa ni michango ya wanachama, shilingi bilioni 32.13 mapato yanayotokana na uwekezaji katika vitega uchumi, shilingi bilioni 81.81 vitega uchumi vilivyo komaa, shilingi bilioni 21.95 marejesho ya mikopo kutoka kwa wanachama na shilingi bilioni 5.21 ni mapato kutokana na vyanzo vingine. Mfuko ulifanikiwa kutoa huduma ya mikopo ya elimu, mikopo ya kujipanga kimaisha kwa wanachama na mikopo ya viwanja kwa yenye thamani ya shilingi

bilioni 1.14 kwa wanachama 618 kupitia mabenki mbalimbali.

### (ii) Mfuko wa Mafao ya Kustaafu wa GEPF

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2017 hadi Aprili, 2018 Mfuko umesajili jumla ya wanachama 20,395 sawa na asilimia 57 ya lengo la kusajili wanachama 36,049 kwa mwaka. Ukusanyaji wa michango kutoka kwa wanachama ilifikia shilingi bilioni 64.48 sawa na asilimia 71 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 90.35 kwa mwaka. Makusanyo ya mapato yatokanayo na vitega uchumi yalifikia shilingi bilioni 35.14 sawa na asilimia 52 ya lengo la kukusanya jumla ya shilingi bilioni 67.06 kwa mwaka. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2018 thamani ya Mfuko ilifikia shilingi bilioni 605.9 sawa na asilimia 94 ya lengo la shilingi bilioni 645.34.

### (iii) Mfuko wa Pensheni wa PPF

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Pensheni wa PPF kwa kipindi cha Julai, 2017 hadi Aprili, 2018 umetekeleza yafuatayo: kuandikisha wanachama 51,211 sawa na asilimia 44 ya lengo la kuandikisha wanachama 116,502; kukusanya shilingi bilioni

337.29 kutoka kwa wanachama wake ikiwa ni sawa na asilimia 71 ya malengo la kukusanya bilioni 473.5; uwekezaji katika vitega uchumi ulifikia shilingi trilioni 2.39 kati ya trilioni 2.48; mapato kutokana na uwekezaji yalifikia shilingi bilioni 257.49 sawa na asilimia 96 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 268.18. Aidha, shilingi bilioni 237.27 zimetumika kulipia mafao sawa na asilimia 88 ya lengo la kulipa shilingi bilioni 270.77. Vile vile, na thamani ya mfuko hadi Aprili 2018 iliongezeka na kufikia shilingi trilioni 2.78 ikiwa ni ongezeko la asilimia 12.10 kutoka thamani ya mfuko ya shilingi trilioni 2.48 iliyokuwepo Juni 2017.

### 3.5.3 Rufani za Kodi

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuanzia Julai, 2017 hadi Aprili, 2018 Bodi ya Rufani za Kodi (TRAB) imesajili jumla ya kesi 436 ambapo kesi 147 zimesikilizwa na kutolea maamuzi. Kati ya hizo, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeshinda kesi 111 zenye jumla ya shilingi bilioni 535.2 na Dola ya kimarekani milioni 38.4 na walalamikaji wameshinda kesi 37 zenye jumla ya shilingi bilioni 35. Aidha, katika kipindi hicho TRAB imekusanya

kesi zilizoamuliwa kuanzia mwaka 2011-12 ili kuchapisha "Tanzania Tax Law Reports" za mwaka kwa ajili ya rejea kwa wadau wa kodi. Vile vile, Baraza la Rufani za Kodi (TRAT) limesajili jumla ya kesi 106 (kati ya hizo kesi 43 zilibaki bila kutolewa maamuzi katika mwaka 2016/17). Hadi Aprili, 2018 jumla ya kesi 62 zimesikilizwa na kutolewa maamuzi na kesi 44 bado zinaendelea kusikilizwa, kati ya hizo TRA imeshinda kesi 26 zenye jumla ya shilingi bilioni 63.87 na Dola ya kimarekani milioni 17.98 na walalamikaji wameshinda kesi moja yenye thamani ya shilingi milioni 455.32.

### 3.5.4 Huduma za Bima

#### (i) Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA)

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2018, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima imefanya marekebisho madogo ya Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009 yenye mabadiliko ya kimfumo na kiutawala katika usimamizi wa soko la Bima. Mabadiliko hayo ni pamoja na kuweka masharti kwa waagizaji wote wa bidhaa na mizigo inayoingizwa nchini kukatia bima kupitia kampuni za ndani na tozo za bima kulipwa moja kwa moja kwa kampuni za bima kutoka kwa madalali. Aidha,

Mamlaka imeandaa kanuni za uuzaji na utoaji wa Bima za Kiislam (Takaful Insurance) ambazo zipo katika hatua ya kuidhinishwa na imeanzisha Mifumo ya Kieletroniki ya Usimamizi wa soko la Bima.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Uelimishaji wa Masuala ya Bima (National Insurance Education Strategy (NIES) 2016 - 2020). Mkakati huu utatoa fursa ya kutoa elimu kwa umma katika ngazi mbalimbali ikiwemo shule za msingi na sekondari, vyuo vya elimu juu, taasisi za dini na vikundi mbalimbali vya kijamii. Tayari Mamlaka imepokea fedha kiasi cha Dola ya Marekani 180,000 kutoka *Financial Sector Deepening Trust* (FSDT) kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanapewa elimu ya bima.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa wananchi ya ucheleweshaji wa fidia pale wapatwapo na majanga, kuwepo kwa bima ghushi katika vyombo vya moto na mapunjo katika fidia. Ili kushughulikia malalamiko hayo, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Nchini (TIRA) imeweka mifumo ya kielektroniki ya kupokea malalamiko na kuyafanyia kazi; Mamlaka

imeanzisha programu tumizi ya simu iitwayo TIRA MIS yaani *Tanzania Insurance Regulatory Authority Manangement Information System* ili kuwarahisishia wananchi kuhakiki uhalali wa bima za vyombo vya moto; na kufanya kazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima ili kuamua malalamiko ya wananchi yahusuyo kiwango cha fidia.

**(vi) Shirika la Bima la Taifa (NIC)**

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2017 hadi Aprili, 2018 Shirika la Bima la Taifa limefanikiwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 62.51 sawa na asilimia 69 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 90.48. Makusanyo haya yanajumuisha mapato kutokana na ada za bima shilingi bilioni 54.05, mapato kutokana na vitega uchumi shilingi bilioni 4.87, na mapato kutokana na Bima Mtawanyo (reinsurance) shilingi bilioni 3.59.

### 3.5.5 Mitaji na Dhamana

**(i) Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)**

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo ya mitaji ya Umoja wa Mataifa (United Nations Capital Development Fund-UNCDF) imefanya mazungumzo na Mamlaka ya Serikali za Mitaa juu ya fursa za utoaji wa hatifungani kwa kutumia Masoko ya Mitaji, kwa kuuza hatifungani za Serikali za Mitaa yaani 'Municipal Bonds' ili kupata fedha za miradi ambayo inaweza kujiendesha yenyewe ili kuleta tija kijamii na kiuchumi. Mpaka sasa elimu imetolewa kwa Halmashauri za Manispaa za mkoa wa Mwanza, Tanga na Arusha na juhudi zinafanyika ili elimu itolewe kwa Halmashauri zote nchini.

**94.** ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kuongeza wataalamu wenye weledi na ujuzi kwa ngazi ya kimataifa kwenye masoko ya mitaji, Mamlaka kwa kushirikiana na Taasisi ya Uwekezaji na Dhamana (Chartered Institute for Securities and Investment – CISI, London UK) ya Uingereza iliendesha mafunzo yanaotambulika kimataifa kwa wataalamu 60 ambayo yamewezesha kujenga uwezo na ufanisi kwa watendaji wa masoko ya mitaji. Hatua hiyo inatarajia kuwezesha

wawekezaji wa kimataifa kuongeza imani juu ya masoko yetu.

**95.** ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka iliendelea kutoa elimu kwa umma ili kuongeza uelewa na ushiriki wa wananchi katika masoko ya mitaji kwa kuendesha semina kwa wataalamu 7,872 wa kada mbalimbali na waheshimiwa wabunge 60 kuhusu Masoko ya Mitaji na Dhamana. Aidha, Mamlaka imeandaa rasimu ya marekebisho ya sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana na kuwasilishwa kwa wadau ili kupata maoni ambayo yatajumuishwa kwenye rasimu hiyo.

### (ii) Soko la Bidhaa Tanzania – Tanzania Commodity Exchange Market

**96.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18 Soko la Bidhaa Tanzania liliendelea kukusanya mtaji ambapo kiasi cha shilingi bilioni 4.5 kimepatikana kutoka kwa wanahisa watatu ambao ni Msajili wa Hazina, Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma (PSPF) na Benki ya Maendeleo ya TIB. Aidha, Bodi ya Wakurugenzi ya Kudumu imeteuliwa. Mshauri Mkazi wa uendeshaji wa Soko la Bidhaa ameanza kazi ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa Soko la

Bidhaa. Vilevile, ofisi na sakafu ya biashara (trading floor) ya Soko la Bidhaa zimeshakamilika tayari kwa kuanza biashara kwa mfumo wa utamkaji bei hadharani (Public Open Outcry). Soko la Bidhaa litaanza biashara kwa mfumo wa utamkaji wa bei hadharani ili kujenga ufahamu kwa washiriki na wadau wake muhimu juu ya kinachofanyika katika soko la bidhaa kabla ya kuhamia kwenye mfumo wa kielektroniki.

**97.** ***Mheshimiwa Spika***, Soko la Bidhaa Tanzania limesajili kampuni tano (5) za uwakala wa Soko la Bidhaa (market intermediaries) ambao watatoa huduma ya kuwaunganisha wanunuzi na wauzaji bidhaa. Kampuni hizo ni Buyuni Futures and Multicommodities LTD; Zani Mercantile LTD; Fidelity Capital Ltd; Lake Commodities LTD; na Solomon Commodities LTD. Aidha, benki sita (6) ambazo baada ya tathmini zilionekana kukidhi vigezo vikiwemo vya kuwa na mtandao mpana wa matawi, hali nzuri ya kifedha na uzoefu wa utoaji huduma katika masoko ya bidhaa na fedha zimeidhinishwa kutoa huduma kwenye soko la bidhaa. Benki hizo ni CRDB Bank, NMB Bank, Standard Chartered, TIB Corporate Bank, Exim Bank na Azania Bank. Vile vile, kwa kushirikiana Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi Ghalani, Wizara

ya Kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara na Bodi ya Mazao Mchanganyiko imeandaa mikataba elekezi (*contract specifications*) ya bidhaa zitakazouzwa sokoni. Mazao ambayo mikataba yake imeandaliwa na kuidhinishwa na Bodi na Mamlaka husika ni pamoja na ufuta, alizeti, korosho, mahindi, mbaazi, njugu mawe, soya, na mchele. Soko la Bidhaa pia limeanzisha utayarishaji wa rasimu ya mikataba ya mazao ya madini kama Dhahabu ambayo yanategemewa kuuzwa kwenye soko hilo.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** Soko la Bidhaa kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya TIB, Mamlaka ya Masoko na Mitaji – CMSA, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania – TADB, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala – WRRB na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania – TCDC ilipitia maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa Pamba katika mikoa ya Mwanza, Simiyu, Shinyanga na Geita ili kuangalia namna nzuri ya kuanzisha mfumo wa stakabadhi za Ghala na kuuza kupitia Soko la Bidhaa. Baada ya kukagua miundo mbinu ikiwemo ghala na vinu vya kuchambulia pamba na pia hali ya madeni ya vyama vya ushirika, ilibainika kuwa katika kipindi cha muda mfupi mfumo wa stakabadhi za Ghala unaweza kuanzishwa katika

wilaya za Chato na Kahama wakati changamoto zinazokabili maeneo mengine zikifanyiwa kazi. Soko la Bidhaa na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala kwa kushirikiana na wadau wengine imeshaanza maandalizi ya kuingiza zao la pamba katika mfumo wa stakabadhi za ghala na kuandaa mkataba elekezi wa zao la pamba ili kuwezesha pamba kuuzwa kwenye soko la bidhaa.

### (iii) Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE)

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** Soko la Hisa Dar es Salaam limeendelea kuwezesha upatikanaji wa fedha za muda mrefu za mitaji na utoaji wa fursa za uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2018 idadi ya kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa Dar es Salaam ziliongezeka kutoka 25 hadi 27. Kati ya hizo 20 ni kampuni za ndani na saba (7) ni kampuni za nje zilizoorodheshwa kwenye masoko ya hisa ya Nairobi na London. Aidha, Serikali imeorodhesha hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 2,943 mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia 80 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,635 mwaka 2016. Kwa ujumla, hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa hadi Machi

2018 ni shilingi bilioni 8,477. Kwa upande wa kampuni binafsi, hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 122 zilikuwa zimeorodheshwa katika soko. Vile vile, thamani ya hisa zilizopo sokoni ilikuwa ni shilingi bilioni 23,199, ambapo shilingi bilioni 10,729 ni za kampuni za ndani.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2017, hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 516 ziliuzwa na kununuliwa. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 23 ikilinganishwa na hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 421 zilizouzwa na kununuliwa katika Mwaka 2016. Kwa upande wa hatifungani, katika mwaka 2017 hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 684 ziliuzwa na kununuliwa. Hili ni ongezeko la takribani asilimia 60 ikilinganishwa na hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 426 zilizouzwa na kununuliwa katika mwaka 2016. Aidha, kama sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya EPOCA, inayotaka kampuni za simu kuuza asilimia 25 ya hisa kwa umma na kujiorodhesha katika soko la hisa, DSE iliweza kuorodhesha kampuni ya Vodacom Tanzania Ltd iliyouza hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 476. Vile vile, DSE ilipokea maombi kutoka kampuni nyingine nne (4) ambazo zipo katika hatua mbalimbali za kupata ruhusa ya

kuorodheshwa. Kampuni hizo ni TCCIA Investment, Tigo, Airtel na Zantel.

### 3.5.6 Dhamana za Uwekezaji Tanzania

#### (i) Taasisi ya Huduma za Fedha na Mikopo Tanzania (UTT MFI)

**101.** ***Mheshimiwa Spika*,** Taasisi ya Huduma za Fedha na Mikopo Tanzania (UTT MFI) imeendelea na jukumu la kutoa huduma shirikishi za kifedha na mikopo ya aina mbalimbali kwa Watanzania wenye kipato cha chini na cha kati. Hadi kufikia Aprili 2018, Taasisi imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.35 kwa wafanyakazi wa Umma, wafanyabiashara na wakulima wapatao 7,250 kwa lengo la kujikwamua kimaisha. Taasisi imeweza kuingiza mapato ya shilingi bilioni 0.98 yakiwa ni kutokana na riba, tozo za usajili, tozo za bima, kamisheni za uwakala na mapato mengineyo.

#### (ii) Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji (UTT AMIS)

**102.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2017/18, Kampuni ya UTT AMIS iliendelea kutekeleza jukumu la kusimamia mifuko ya uwekezaji wa

pamoja na kutoa huduma za ushauri katika uwekezaji. Hadi kufikia Aprili 2018, mifuko pamoja na huduma ya usimamizi mitaji binafsi ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 283.19 ikilinganishwa na shilingi bilioni 253.29 Juni 2017. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 11.8 na jitihada zinafanyika ili kufikia lengo la mwaka la asilimia 15. Aidha, taasisi iliongeza idadi ya wawekezaji kutoka 135,178 Juni 2017 hadi 139,806 Aprili 2018 ikiwa ni ongezeko la wawekezaji 4,628 ambalo ni sawa na asilimia 3.4 ikilinganishwa na lengo la mwaka la asilimia 5. Idadi hii ya wawekezaji inajumuisha watu binafsi na mashirika na vikundi.

### (iii) Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu (UTT PID)

**103.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Miradi ya Maendeleo ya Miundombinu (UTT PID) hadi kufikia Aprili, 2018 imetekeleza yafuatayo:- kuandaa maandiko ya miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 10 ya kupima viwanja maeneo ya Jiji la Dodoma, Chamwino, Ifakara, Mwasonga (Kigamboni); kuingia mkataba na Mamlaka ya Bandari (TPA) katika kushauri na kusimamia shughuli zote za ujenzi zinazoendelea kwenye jengo jipya la ghorofa 35. Aidha, mauzo ya viwanja

vipatavyo 2,450 vyenye thamani ya shilingi bilioni 5 yanaendelea katika maeneo ya Kahama, Bukoba, Sengerema, Morogoro, Lindi, Bagamoyo, Chalinze na Kigamboni.

### 3.5.7 Taasisi za Mafunzo

#### (i) Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM)

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kimeendelea kutoa mafunzo katika matawi yake yaliyoko Dar es Salaam na Mwanza katika fani mbalimbali zikiwemo: Usimamizi wa Fedha; Uhasibu; Benki; Bima; Kodi; Hifadhi za Jamii; Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari (ICT); na Sayansi ya Kompyuta. Katika mwaka 2017/18 jumla ya wanafunzi 9,711 wamedahiliwa ikilinganishwa na wanafunzi 8,559 mwaka 2016/17. Aidha, Chuo kimeanzisha mafunzo ya "Masters of Science in Finance and Investment" yanayotolewa na wahadhiri wa IFM katika majengo ya Chuo cha Mipango Dodoma ili kutoa fursa kwa watumishi wa Serikali na wengine waliopo Dodoma kupata mafunzo.

## (ii) Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP)

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Chuo kilidahili wanafunzi 3,591 ikilinganishwa na wanafunzi 2,639 mwaka 2016/17. Aidha, katika mahafali yake ya 31 ya mwaka 2017/18 jumla ya wahitimu 3,108 wakiwemo wanaume 1,477 na wanawake 1,631 walihitimu mafunzo yao katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada ya kwanza, Stashahada ya uzamili na Shahada ya Uzamili katika kozi za mipango ya maendeleo vijijini. Kadhalika, chuo kinaendelea na utekelezaji wa miradi na tafiti mbalimbali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo wakiwemo Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo (IIED) ya Uingereza, Umoja wa Ulaya, Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID) na "Alliance for Green Revolution in Africa" (AGRA). Lengo la miradi hiyo ni kuhakikisha mafunzo ya nadharia yanayotolewa darasani kwenda kwenye uhalisia katika jamii zetu. Aidha, chuo kimewawezesha wafanyakazi wake 27 kuendelea na mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali za kitaaluma katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

### (iii) Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA)

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2017/18 Chuo cha Uhasibu Arusha kimetekeleza yafuatayo: kudahili wanafunzi 3,849 ikilinganishwa na wanafunzi 3,718 waliodahiliwa mwaka 2016/17; kupitia mitaala yote baada ya kutumika kwa miaka mitatu mfululizo na kuiwasilisha NACTE; Kuanza kutoa mafunzo ya Shahada ya Sayansi ya Kijeshi (Bachelor in Military Science) na Stashada ya Uzamili ya Sayansi ya Kijeshi kwa kushirikiana na Tanzania Military Academy (TMA); kuanza kufundisha kwa kutumia mtandao (Moodle) kwa shahada ya Uzamili ikiwa ni hatua muhimu ya kuanzisha kituo cha Elimu masafa (Distance - Learning Centre); na kufadhili watumishi kwa ngazi ya Shahada ya Uzamivu (PhD) ambapo walimu 10 wapo masomoni.

### (iv) Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA)

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hadi Aprili, 2018 Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: Kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka 14,424 mwaka 2016/17 hadi 14,550 mwaka 2017/18; kuongezeka kwa wanafunzi wanaohitimu kwa kiwango cha daraja la kwanza na la pili kutoka

wanafunzi 384 mwaka 2003/04 hadi wanafunzi 2,860 mwaka 2016/17; Kuongezeka mapato ya Taasisi kutoka shilingi bilioni 15 mwaka 2015/16 hadi shilingi bilioni 17 mwaka 2017/18 hivyo kuongeza uwezo wa kujitegemea kwa zaidi ya asilimia 70; na Kupata hati safi ya ukaguzi kwa miaka mitano (5) mfululizo.

## (v) Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC)

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) kimeendelea kutoa mafunzo ya takwimu rasmi na takwimu za kilimo kwa ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili. Udahili wa wanafunzi umeongezeka kutoka wanafunzi 323 mwaka 2016/17 hadi kufikia wanafunzi 415 mwaka 2017/18. Chuo kimeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), *Italy Development Agency* na Shirika la DAAD la Ujerumani katika kuendesha mafunzo kwa wanataaluma, watakwimu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na udhamini wa wanafunzi.

### 3.5.8 Taasisi za Kitaalam na Huduma Nyinginezo

#### (i) Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka 2017/18 Mamlaka ya Mapato Tanzania ilipanga kukusanya shilingi bilioni 17,106.33 kwa Tanzania Bara sawa na ongezeko la asilimia 21 ikilinganishwa na makusanyo halisi katika mwaka 2016/17. Hadi Aprili 2018, mapato halisi ya kodi Tanzania Bara yalifikia shilingi bilioni 12,603.01 ikilinganishwa na lengo la kukusanya shilingi bilioni 14,225.44, sawa na ufanisi wa asilimia 88.6. Aidha, makusanyo haya ni sawa na ongezeko la asilimia 8.2 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 11,644.68 zilizokusanywa katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2016/17. **Jedwali Na. 4.**

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Zanzibar, Mamlaka ilipanga kukusanya shilingi bilioni 258.72 sawa na ongezeko la asilimia 26.9 ikilinganishwa na makusanyo halisi ya Mwaka 2016/17. Hadi Aprili 2018, makusanyo yalifikia shilingi bilioni 210.26 ikilinganishwa na lengo la kukusanya shilingi bilioni 213.97. Makusanyo hayo

ni sawa na ufanisi wa asilimia 98.3 ya lengo ikilinganishwa na shilingi bilioni 152.6 sawa na ongezeko la asilimia 24.8 ya makusanyo katika kipindi kama hicho mwaka 2016/17. **Jedwali Na. 5.**

## (ii) Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha kuanzia Julai 2017 hadi Aprili, 2018 Ofisi ya Taifa ya Takwimu imefanya kazi za kukusanya, kuchambua, kutunza na kuwasilisha takwimu rasmi zinazohitajika katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa wakati kama ifuatavyo:- Mfumuko wa bei mwezi Julai, 2017 hadi Aprili 2018; Pato la Taifa kila robo mwaka na Takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka 2017; Fahirisi za bei za uzalishaji bidhaa viwandani hadi robo ya tatu ya mwaka 2017; Fahirisi za uuzaji na uagizaji wa bidhaa nje ya Nchi; Matokeo muhimu ya Utafiti wa Viashiria na Matokeo ya Ukimwi Tanzania wa mwaka 2016/17; Makadirio ya idadi ya watu kwa umri kwa mwaka 2013 hadi 2035; Ripoti ya Takwimu za kodi 2015/16; Takwimu za uhalifu na makosa ya usalama barabarani 2017; Utafiti wa ajira na

mapato, 2016 (Sekta rasmi); na Tafiti za Sekta ya Utalii Tanzania 2017.

### (iii) Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA)

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu imeendelea kutekeleza majukumu mbalimbali kwa kufanya yafuatayo: Kuweka na kusimamia viwango vya Uhasibu na Ukaguzi; Kufanya uhariri wa mitaala na silabi ya Taaluma ya uhasibu; kuendeleza taaluma ya uhasibu kwa kutunga, kusimamia na kusahihisha mitihani ya ngazi ya cheti na CPA (T); kuendelea kutoa huduma za maktaba na machapisho kuhusu shughuli za NBAA kwa wadau katika jarida la "The Accountant"; kutoa mafunzo endelevu kwa wanataaluma ambapo hadi Aprili, 2018 jumla ya semina 16 ziliendeshwa zenye jumla ya washiriki 7,709; kusimamia ubora wa ukaguzi wa hesabu ambapo jumla ya kampuni 54 zilifanyiwa ukaguzi wa ubora; na kusajili jumla ya wahasibu 980. Aidha, hadi Aprili, 2018 Bodi imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 9.11 kutoka vyanzo mbalimbali.

### (iv) Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (Gaming Board)

**113.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18, Bodi imeendelea kusimamia, kuratibu na kutoa leseni za michezo ya kubahatisha. Hadi Aprili, 2018, Bodi ilifanya ukaguzi kwa waendeshaji wa michezo ya kubahatisha ili kuhakikisha kuwa michezo hiyo inaendeshwa kwa kuzingatia matakwa ya sheria za nchi. Aidha, Bodi inaendelea kufuatilia kwa karibu na kuhakikisha kwamba kodi stahiki inayotokana na michezo ya kubahatisha inakokotolewa na kulipwa TRA.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imeendelea kuhakikisha kwamba jamii yetu inalindwa ipasavyo dhidi ya athari mbaya inayoweza kusababishwa na uwepo wa michezo hii. Katika kutekeleza wajibu huu, Wizara kupitia Bodi ya Michezo ya Kubahatisha imesimamia vyema Sheria inayokataza watoto kushiriki katika michezo hii. Hali kadhalika, Bodi imechukua hatua kuhakikisha kuwa matangazo ya michezo hii inadhibitiwa na kuwa ya kiasi ili kusiwepo na ushawishi uliopitiliza kwa jamii, na hasa vijana kushiriki katika michezo hii na kufanya kuwa chanzo kikuu cha mapato yao.

Bodi itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuhakikisha kwamba sekta hii inaendelea kuwa ya burudani lakini huku ikichangia ipasavyo katika maendeleo ya nchi yetu.

**(v) Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha (SELF Microfinance Fund)**

**115.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Aprili 2018, Mfuko wa SELF umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 18.25 ikilinganishwa na lengo la kutoa shilingi bilioni 20. Mikopo hiyo imetolewa kwa Asasi za fedha 61 ambapo 30 ni SACCOS, 26 ni kampuni za fedha na 5 ni benki za jamii. Mikopo hiyo iliwanufaisha wajasiriamali wadogo 15,089, kati ya hao 9,011, sawa na asilimia 60 ni wanawake na 6,078 ni wanaume sawa na asilimia 40. Mfuko umegharamia mafunzo kwa vitendo kwa watendaji 66 wa Asasi 30. Mfuko umekusanya mapato ya shilingi bilioni 3.08 sawa na asilimia 47.4 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 6.5.

### 3.5.9 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo mwaka 2017/18

#### (i) Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/18, Wizara ilianza utekelezaji wa Awamu ya Tano ya Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma baada ya utekelezaji wa Awamu ya Nne kukamilika 2016/17. Programu hii inalenga kutatua changamoto mbalimbali katika usimamizi wa fedha za umma ikiwa ni pamoja na ukadiriaji wa vyanzo vya mapato na mtiririko wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali; kuunganisha mifumo ya fedha katika Serikali Kuu na Mamlaka ya Serikali za Mitaa; usimamizi wa mali za Serikali; usimamizi wa mapato na matumizi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa; udhibiti wa ndani na ununuzi wa Umma; uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia programu hii, Wizara imetekeleza yafuatayo: kukamilisha zoezi la tathmini ya usimamizi wa fedha kwa kufuata viwango vya kimataifa kwa mwaka 2017 (Public Expenditure and Financial Accountability

Assessment – PEFA 2017), tathmini hiyo ilionyesha kuwa usimamizi wa fedha za umma umeendelea kuimarika; kuwajengea uwezo watumishi wa kada za fedha, ununuzi wa umma, TEHAMA; ukaguzi wa ndani na usimamizi wa rasilimali za Serikali kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea na Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kusimamia fedha na mali ya umma; Kukamilika kwa maandalizi ya uanzishwaji wa ununuzi wa Umma kwa njia ya kieletroniki (e-procurement); Kuendelea kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji fedha katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa; na kukamilika kwa Sera ya Usimamizi wa Mali za Serikali na Mpango Mkakati wa utekelezaji wake.

### (ii) Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Kuimarisha na Kuboresha Takwimu Tanzania (TSMP)

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inaendelea na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kuimarisha Takwimu Nchini- (Tanzania Statistical Master Plan - TSMP). Lengo kuu la Mradi huu ni kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na usambazaji wa Takwimu rasmi nchini. Katika mwaka 2017/18, NBS imekamilisha ujenzi wa jengo la makao makuu ya Ofisi ya Taifa

ya Takwimu katika Jiji la Dodoma (Takwimu House). Aidha, shughuli nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na kukusanya, kuchambua, kutunza na kuwasilisha takwimu rasmi zinazohitajika katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

### (iii) Kusaidia Ufanisi wa Bajeti za Wizara na Idara za Serikali (MDAs Performance Budget Support)

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2018, Wizara kupitia mradi wa kusaidia bajeti za Wizara na Idara za Serikali imeongeza mtaji wa shilingi bilioni 50 kwa benki ya *TIB Development.* Lengo ni kuiwezesha benki hiyo kugharamia utekelezaji wa miradi mikubwa inayoweza kujiendesha kibiashara. Aidha, mradi umeendelea kulipa madeni yaliyohakikiwa katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1,167.7 zimelipwa.

## 3.6 CHANGAMOTO NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA

### 3.6.1 CHANGAMOTO

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara, changamoto zilizojitokeza ni pamoja na:

i. Ukwepaji wa kodi na kutokulipa kodi kwa hiari;
ii. Kuchelewa kupatikana kwa misaada na mikopo ya masharti nafuu pamoja na mikopo ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
iii. Uelewa mdogo wa watoa taarifa na umma juu ya dhana ya utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi ambayo ni pana na inabadilika kwa kasi;
iv. Baadhi ya wawekezaji kutelekeza mali walizouziwa na Serikali wakati wa zoezi la Ubinafsishaji; na
v. Uelewa mdogo wa dhana ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa mamlaka za utekelezaji wa miradi ya ubia.

### 3.6.2 HATUA ZA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa bajeti kama zilivyobainishwa hapo juu, Wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo:

i. Kutekeleza mkakati wa ulipaji kodi kwa hiari na kuendelea kuboresha makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi kwa kujenga mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato;

ii. Kuwianisha mapato na matumizi katika kutenga fedha za matumizi na kuendelea kusisitiza na kuelimisha mazingatio ya matumizi ya Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 na kanuni zake;

iii. Kufuatilia utekelezaji wa masharti ya makubaliano ya mikataba ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili fedha zilizoahidiwa zitolewe kwa wakati;

iv. Kuendelea kuelimisha wadau mbalimbali kupitia makongamano, mikutano na warsha kuhusu dhana ya utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi;

v. Kuendeleza mazungumzo na Washirika wa Maendeleo kuhusu njia mpya za kutoa na

kupokea misaada na mikopo (*New Financing Instruments);*

vi. Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imeongeza nguvu katika kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa wawekezaji wote ili kuhakikisha wanaendesha viwanda na mali walizouziwa kwa kuzingatia Masharti ya Mikataba ya Mauzo; na

vii. Kuendelea kutoa mafunzo ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na sekta binafsi.

## 4.0 MALENGO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2018/19

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kueleza utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2017/18, naomba niwasilishe malengo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2018/19.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2018/19 umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka

Mitano (2016 /17- 2020/21), Sheria ya Bajeti Na.11 ya Mwaka 2015, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi – CCM (2015 – 2020), Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa Uzinduzi wa Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na masuala mtambuka kama vile Jinsia, watu wenye ulemavu, Mazingira, UKIMWI, makundi mengine yaliyo katika mazingira hatarishi na masuala ya lishe kwa jamii pamoja na maelekezo na ahadi zilizotolewa Kitaifa.

## 4.1 MPANGO WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA

### 4.1.1 Kubuni na Kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Uchumi Jumla

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** shabaha za uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2018/19 ni kama ifuatavyo:-

(i) Pato la Taifa kukua kwa asilimia 7.2 mwaka 2018 kutoka ukuaji halisi wa asilimia 7.1 mwaka 2017;

(ii) Mfumuko wa bei kuendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19 kutoka matarajio ya

asilimia 15.3 mwaka 2017/18 na asilimia 15.6 mwaka 2016/17;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.6 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19 kutoka matarajio ya asilimia 13.0 mwaka 2017/18 na asilimia 13.3 mwaka 2016/17; na

(v) Nakisi ya bajeti kufikia asilimia 3.2 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19 kutoka matarajio ya asilimia 2.1 mwaka 2017/18 na asilimia 1.5 mwaka 2016/17.

### 4.1.2 Uratibu wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuunganishwa kwa iliyokuwa Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha, imebidi kuupitia muundo wa Wizara uweze kuyaingiza mabadiliko haya ili kutoathiri utekelezaji wa majukumu pamoja na maslahi ya watumishi kwa ujumla. Muundo wa Wizara uko katika hatua za mwisho za kuidhinishwa na Mamlaka husika.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** hivyo katika mwaka 2018/19, shughuli za kipaumbele zitakazotekelezwa katika uratibu wa mipango ya maendeleo ya Taifa ni pamoja na: Kuandaa

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20; Kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2018/19; Kufanya tathmini ya muda wa kati katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; Kukamilisha uundwaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa usimamizi wa miradi ya kitaifa ya Maendeleo; na Kufuatilia matumizi ya Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma (Public Investment Management - Operational Manual - PIM – OM).

### 4.1.3 Uratibu wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini

**127.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19, Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa juhudi za kupunguza umaskini ikiwemo kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji wa Jitihada za Kuondoa Umaskini nchini (Poverty Monitoring System - PMS); kufuatilia utekelezaji wa malengo yaliyoainishwa katika Mipango ya kitaifa na kisekta na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030 na programu zinazolenga kuondoa umaskini katika maeneo ya vijijini na mijini; kufanya uchambuzi wa kina juu ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS-2017/18); kutoa mafunzo kwa Maafisa Mipango na

Maendeleo ya Jamii wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhusu jitihada za kupambana na umaskini na kutunza mazingira ili kuweza kujumuisha katika mipango na bajeti zao.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itafanyia majaribio Mwongozo wa Mfumo wa Kuibua Fursa na Kukuza Maendeleo ya Uchumi katika ngazi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Local Economic Development Guideline - LED) katika baadhi ya Halmashauri nchini ili kuleta ushiriki wa Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na Wadau wote wa maendeleo. Changamoto zitakazoibuliwa wakati wa majaribio zitasaidia kurekebisha kasoro kabla ya kuanza kutumika. Jitihada hii itasaidia kuwajengea uwezo Maafisa Mipango na Maendeleo ya Jamii wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa nchini ili kuongeza ufanisi na pia kuongeza ushiriki wa wananchi katika miradi ya uzalishaji yenye tija katika kujiongezea vipato hususan vijijini.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaratibu maandalizi ya Taarifa ya Mapitio ya Kitaifa ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2030) itakayowasilishwa katika mkutano wa jukwaa la kisiasa la ngazi ya juu (UN High Level Political Forum) la Umoja wa Mataifa Julai, 2019. Nchi

mbalimbali duniani zitakutana kujadili maendeleo ya utekelezaji wa SDGs 2030, changamoto na kubadilishana uzoefu juu ya kukabiliana na changamoto hizo na uboreshaji zaidi wa mipango ya maendeleo.

### 4.1.4 Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

#### (a) Mapato ya Ndani

**130.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa mwaka 2018/19, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo: kusimamia sera za fedha na kibajeti zinazolenga kuimarisha uwekezaji na biashara; kusimamia dhana ya kulipa kodi kwa hiari kwa kuimarisha Mkakati Shirikishi wa Mawasiliano na Walipa kodi na kuboresha utaratibu wa utozaji kodi ya mapato kwa wafanyabiashara wadogo; kujenga uwezo wa watumishi ili kukabiliana na tatizo la uhamishaji faida (Transfer Pricing) unaofanywa na kampuni zenye mitandao ya kimataifa kwa lengo la kukwepa au kupunguza kodi; kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa ulipaji kodi kupitia Mfumo wa Vitalu vya Walipakodi; kusimamia zoezi la uunganishaji wa Wizara, Idara, Wakala, taasisi na

mashirika ya umma kwenye Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato (GePG) ili kuboresha ukusanyaji na kudhibiti upotevu wa mapato ya Serikali; na kuongeza kasi ya uthaminishaji wa majengo ili kuongeza mapato yatokanayo na kodi ya majengo.

**131.** ***Mheshimiwa Spika***, mikakati mingine iliyopangwa kutekelezwa na Wizara katika kuongeza mapato ya ndani ni pamoja na: kuimarisha usimamizi na ukaguzi kwenye kampuni ambazo Serikali ina hisa ili kuhakikisha kuwa Serikali inapata gawio stahiki katika uwekezaji wake; na kuimarisha usimamizi katika Mashirika na Taasisi za umma ili kuhakikisha kuwa Sheria ya Fedha ya mwaka 2015 na Sheria ya Msajili wa Hazina ya mwaka 1959 na marekebisho yake ya mwaka 2002 na mwaka 2010 inatekelezwa kikamilifu. Sheria hiyo inaelekeza Mashirika na Taasisi za Umma kuchangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali asilimia 15 ya mapato ghafi na asilimia 70 ya ziada inayobaki baada ya matumizi.

### (b) Misaada na Mikopo

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19 Wizara itaendelea na uratibu wa upatikanaji wa

fedha za misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kugharamia programu na miradi ya maendeleo mbalimbali nchini. Washirika wa Maendeleo wameahidi kuchangia Bajeti ya Serikali kiasi cha shilingi bilioni 2,676.64. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 545.76 ni kwa ajili ya Misaada na Mikopo nafuu ya Kibajeti (GBS), shilingi bilioni 125.86 kwa ajili ya Mifuko ya Pamoja ya Kisekta na shilingi bilioni 2005.02 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**133.** ***Mheshimiwa Spika***, kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kukamilisha Mpango Kazi wa kutekeleza Mwongozo mpya wa ushirikiano (*Development Cooperation Framework- DCF*); kutoa elimu ya DCF kwa Washirika wa Maendeleo, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Wizara, Idara Zinazojitegemea na Taasisi na Mashirika ya Umma, Tasisi Binafsi na Waheshimiwa Wabunge ili waweze kupata uelewa na hatimaye kuunga mkono kwa pamoja ajenda ya Maendeleo hapa nchini; na kukagua miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo.

### 4.1.5 Uandaaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19 Wizara imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo: kuendelea kuboresha Mfumo mpya wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti ya Serikali (CBMS) ikiwa pamoja na kurahisisha utoaji na migao ya kila mwezi na kuendesha mafunzo ya mfumo kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Sekretariati za Mikoa; kufanya marekebisho, kuweka kwenye tovuti, kuchapisha na kusambaza nakala 2,200 Vitabu vya Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya mwaka 2018/19 kama yalivyopitishwa na Bunge, kusambaza kuweka kwenye tovuti, kuchapisha na kusambaza Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2019/20, kuandaa, kuweka kwenye tovuti, kuchapisha na kusambaza Kijitabu cha Bajeti ya Serikali Toleo la Wananchi (Citizens Budget); kuandaa na kuweka kwenye tovuti Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali za kila Robo Mwaka; na kuandaa, kuweka kwenye tovuti, kuchapisha Vitabu vya Makadirio ya Matumizi ya Serikali ya mwaka 2019/20 Juzuu (Volume) na kuwasilisha Bungeni na kusambaza kwa Wizara,

Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa kwa Wadau wengine wa Bajeti ya Serikali.

**135.** ***Mheshimiwa Spika***, kazi nyingine zilizopangwa kufanyika ni pamoja na: kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali pamoja na matumizi ya fedha za umma ikiwemo mishahara kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa; na kuendelea kuchambua na kufanya tathimini ya miradi ya kimkakati kwa misingi ya vigezo vilivyopo ili Halmashauri nyingi zaidi ziweze kunufaika na mkakati huu na kuwajengea uwezo watumishi wa Halmashauri kuweza kuibua miradi inayokidhi vigezo. Aidha, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa kwa kuzingatia Mkakati wa Kulipa na Kuzuia Ulimbikizaji wa Madeni ulioandaliwa na Wizara. Kadhalika, Wizara itaendelea kuimarisha uwazi na uwajibikaji kwa kushirikisha wadau kwenye mapitio ya taarifa za utekelezaji wa Bajeti.

### 4.1.6 Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha za Umma

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2018/19, Wizara itaendelea kudhibiti matumizi ya fedha za umma kwa kufanya ufuatiliaji wa uzingatiaji wa miongozo mbalimbali ya ukaguzi wa ndani iliyotolewa na Wizara na kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa ndani katika maeneo ya ukaguzi wa miradi, ukaguzi wa kiufundi, usimamizi wa vihatarishi, mfumo wa usimamizi wa kazi za ukaguzi na mfumo wa kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** mipango mingine ambayo Wizara inatarajia kutekeleza ni pamoja na kufanya ukaguzi maalumu katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, utekelezaji wa bajeti, ukaguzi wa orodha ya mishahara, ukaguzi wa mapato yasiyo ya kodi na ukaguzi wa miradi. Aidha, Wizara inatarajia kufanya uhakiki wa madeni ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Taasisi za Serikali; kufanya

ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na mapendekezo ya wakaguzi wa ndani; na kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani kufanya ukaguzi wa ununuzi na ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia miongozo inayotolewa (Procurement Audit Manual na Contract Management Audit Manual). Aidha, Wizara kupitia Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali itaendelea kufanya uhakiki wa Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund).

### 4.1.7 Usimamizi wa Malipo

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Wizara imepanga kusimamia mfumo wa udhibiti wa matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Akaunti Jumuifu (*Treasury Single Account*) kwa lengo la kuboresha mfumo wa matumizi ya Umma ili kuiongezea Serikali uwezo wa kugharamia shughuli zake kwa wakati. Aidha, Wizara itaendelea na usimikaji na usimamizi wa mifumo ya malipo ya kieletroniki (EFT na TISS) ili kuondoa ucheleweshaji wa malipo kwa wadau mbalimbali wakiwemo wastaafu, watoa huduma kwa Serikali pamoja na watumishi wa Umma. Vile vile, Wizara itaendelea na uunganishaji wa mfumo

wa Malipo (Epicor) kwenye Balozi saba (7) ili kudhibiti uwezekano wa matumizi nje ya bajeti.

### 4.1.8 Deni la Serikali

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Serikali itahakikisha kuwa Deni la Serikali linaendelea kuwa himilivu na kutokuwa mzigo kwa uchumi wetu na kuendelea kuwa fursa na kichocheo cha maendeleo kwa nchi yetu. Aidha, Serikali itaendelea kukopa kwa uangalifu kwa kuzingatia masharti nafuu. Mikopo hiyo itatumika kwenye miradi ya maendeleo yenye vichocheo vya ukuaji wa uchumi ikiwemo; ujenzi wa miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na ujenzi wa mitambo ya kufua umeme.

### 4.1.9 Mchango wa Mwajiri (Serikali) kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuwasilisha kwa wakati michango ya kisheria ya mwajiri ya kila mwezi kwa ajili ya watumishi wa umma kwenye Mfuko Mpya wa Hifadhi ya Jamii utakaochukua nafasi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iliyounganishwa ya PSPF, GEPF, LAPF na PPF pamoja na mifuko ambayo haitaunganishwa ya

NSSF, ZSSF, WCF na Bima ya Afya (NHIF). Natumia fursa hii kuwahakikishia wanachama wa Mifuko itakayounganishwa kuwa haki zao hazitapotea kwa sababu ya kuunganishwa kwa Mifuko hiyo.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninatumia fursa hii kuwasisitiza maafisa utumishi wote wanaohusika na kuingiza taarifa za watumishi wa umma kwenye mfumo wa kompyuta wa kutunza taarifa za watumishi wa umma waingize taarifa za watumishi kwa ukamilifu na usahihi ili uwasilishaji wa michango ya mwanachama na mwajiri kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iwe kamili na sahihi kwa kipindi chote cha utumishi na hatimaye kurahisisha malipo ya mafao, pensheni na mirathi wakati wa hitimisho la utumishi wa umma hivyo kuwaondolea usumbufu watumishi wa umma walioitumikia nchi yao kwa weledi na uaminifu mkubwa.

### 4.1.10 Usimamizi wa Mifumo ya Taarifa za Kifedha

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Wizara imepanga kusimamia na kuboresha uendeshaji na utumiaji wa mfumo wa taarifa za mishahara ya watumishi wa umma (Government

Salaries Payment Platform - GSPP) kwa kuunganisha mfumo huo na taasisi za kibenki na mfumo wa pensheni kwa ajili ya urahisishaji wa huduma za mikopo na pensheni. Aidha, Wizara itaendelea kuunganisha taasisi 260 katika mfumo wa kukusanya mapato yasiyo ya kodi (Government Electonic Payment Gateway System - GePG), ili kuweza kufanikisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Vile vile, Wizara itaunganisha mifumo 10 ya kielektroniki ya taarifa za kifedha kwa lengo la kuiwezesha mifumo iweze kubadilishana taarifa.

### 4.1.11 Usimamizi wa Mali za Serikali

**143.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza jukumu la kusimamia mali za Serikali, katika mwaka 2018/19, Wizara imepanga kufanya kaguzi za mali za Serikali katika balozi kumi (10) za Tanzania, kufanya kaguzi maalum na kutoa elimu ya utumiaji na utunzaji bora wa mali katika taasisi mbalimbali za Serikali ili kuepusha hasara zinazoweza kuzuilika.

### 4.1.12 Ununuzi wa Umma

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Wizara imepanga kufanya yafuatayo: kukamilisha

uandaaji na kuzindua Sera ya Ununuzi wa Umma pamoja kuanza utekelezaji wa sera hiyo; kukusanya maoni ya wadau kuhusu changamoto zinazowakabili katika utekelezaji wa sheria na kanuni za ununuzi wa umma kwa lengo ya kuzifanyia marekebisho pale itakapohitajika; kuwajengea uwezo maafisa ununuzi na ugavi serikalini juu ya matumizi ya mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za ununuzi na ugavi; kuendesha mafunzo kwa maafisa ununuzi na ugavi kuhusu matumizi ya mfumo wa malipo wa EPICOR katika ununuzi; kuandaa mpango kazi wa usimamizi wa ununuzi wa umma katika Serikali Kuu na Mamlaka ya Serikali za Mitaa; na kutekeleza mapendekezo ya taarifa ya tathmini ya ufanisi wa mfumo wa ununuzi wa umma.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizopangwa kufanyika ni pamoja na: kusimamia na kutumia mfumo wa ununuzi wa umma kwa njia ya mtandao - TANePS (*Tanzania National Electronic Procurement*) ili kuongeza ufanisi na uwazi; kufuatilia utoaji na utekelezaji wa mikataba ya ununuzi wa umma; kufanya kaguzi za ununuzi unaofanywa na Taasisi Nunuzi; na kuendelea kutoa elimu na ushauri kwa Taasisi za Umma kuhusu Sheria, Kanuni na taratibu za ununuzi wa umma.

Aidha, Wizara Kupitia Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma imepanga kupokea na kusikiliza Rufaa/Malalamiko 30 yatokanayo na zabuni za umma.

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Wizara kupitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) imepanga kutekeleza yafuatayo: kuendelea na utaratibu wa ununuzi wa magari ya Serikali kwa pamoja; kuendelea kuandaa mikataba maalum ya ununuzi wa vifaa na huduma mtambuka kwa niaba ya Taasisi za Serikali; kuongeza uwezo wa Wakala wa kuhifadhi mafuta katika mikoa ya Mara, Mwanza, Morogoro, Tabora na Mtwara kufikia wastani wa lita 50,000 kila mkoa; kuimarisha uwezo wa Wakala wa kusambaza vifaa na mafuta kwa kununua malori mawili na gari moja (1) kubwa la ujazo wa lita 40,000 kwa ajili ya kusambaza mafuta mikoani; na kuanza ujenzi wa jengo la ofisi za makao makuu ya Wakala mkoani Dodoma pamoja na ujenzi wa ofisi, ghala na kituo cha mafuta katika mkoa wa Geita.

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Bodi ya wataalam wa Ununuzi na Ugavi itaendelea kusimamia mienendo ya Wataalam wa Ununuzi na

Ugavi, kukuza na kuratibu mafunzo na elimu ya fani ya Ununuzi na Ugavi na kutoa ushauri wa kitaalam kwa taasisi za umma na za binafsi kuhusiana na masuala ya Ununuzi na ugavi. Aidha, Bodi imepanga pia kutekeleza yafuatayo: kuingia makubaliano ya ushirikiano na PCCB na Tume ya Maadili kwa ajili ya kushughulikia maadili na kuzuia vitendo vya rushwa; kukuza na kuendeleza taaluma kwa kushirikiana na taasisi ya Ununuzi na Ugavi CIPS (UK) na Taasisi ya Ununuzi na Ugavi ya Kenya (KISM); kusajili wataalam 15,000 na taasisi 20; kuendesha shauri za kitaalam tano (5); kufanya tafiti kumi (10) kwenye nyanja za Ununuzi na Ugavi; kutengeneza kanuni na taratibu za ajira kwenye kada za Ununuzi na Ugavi; na kusajili watahiniwa 25,000 katika mitihani ya Ununuzi na Ugavi.

### 4.1.13 Ukaguzi wa Hesabu za Serikali

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imelenga kuimarisha ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na uwazi kwenye matumizi ya rasilimali za umma. Ili kufikia malengo hayo, Ofisi imepanga kutekeleza vipaumbele nane (8) kama ifuatavyo: kufanya ukaguzi wa mafungu

ya bajeti ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma na Miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na wahisani; kufanya ukaguzi wa sekta ya gesi, mafuta na madini; kufanya maboresho ya mfumo wa ukaguzi kwa kutumia TEHAMA; na kukagua ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi. Aidha, Ofisi imelenga pia kufanya ukaguzi wa kiufanisi na kaguzi maalum katika maeneo yatakayoainishwa; kuwajengea wakaguzi uwezo wa kufanya ukaguzi katika maeneo mapya ya ukaguzi kwenye sekta ya gesi asilia na mafuta, sekta ya madini, Serikali mtandao na katika uhalifu wa kifedha kwa kutumia mtandao (Financial crimes auditing). Vile vile, ofisi itaendelea na ujenzi wa majengo ya Ofisi za Ukaguzi katika Mikoa ya Rukwa na Mara.

#### 4.1.14 Usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imepanga kutekeleza yafuatayo: kufanya mapitio na kufuatilia kampuni ambazo Serikali ina Hisa chache na hazijawasilisha gawio serikalini; kufanya

uchambuzi wa uwekezaji unaofanywa na Mashirika ya Umma katika Kampuni Tanzu na kampuni nyinginezo; kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, kufanya urejeshaji wa viwanda vinavyosuasua na kuwapatia wawekezaji mahiri; kusimamia kwa karibu ukusanyaji wa madeni ya ubinafsishaji wa iliyokuwa Benki ya NBC; kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mifuko ya Jamii, Taasisi za Fedha pamoja na wadau mbalimbali katika suala zima la uwekezaji na ufufuaji wa viwanda, kampuni na mashamba yaliyobinafsishwa.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Msajili wa Hazina itaendelea na ukaguzi wa kimenejimenti kwa taasisi na Mashirika ya Umma; kufanya uchambuzi wa taasisi na Mashirika ya Umma ambayo majukumu yao kwa namna moja au nyingine yanafanana ili kuyaunganisha kwa lengo la kuyaongezea tija na kupunguza gharama za uendeshaji; kuongeza mapato yasiyo ya kodi kwa kuimarisha ufuatiliaji wa ukusanyaji kodi hizo kutoka kwa mashirika na taasisi za umma kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali; kuimarisha usimamizi wa taasisi  na Mashirika ya Umma kwa kuingia mikataba ya utendaji na bodi za taasisi na mashirika; na kufanya uhakiki wa mali za taasisi na

mashirika ya Umma zilizoingizwa katika Daftari la Mali.

### 4.1.15 Mafao ya Wastaafu na Mirathi

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuboresha, kutunza na kusimamia huduma za Pensheni kwa wastaafu wanaolipiwa Hazina ikiwa ni pamoja na kuendelea kulipa kwa wakati mafao na pensheni kwa wastaafu wa Serikali, mirathi kwa warithi na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi wa Serikali walio kwenye mikataba. Aidha, wizara itaendelea kuboresha masijala ya pensheni kwa kuendelea kuhifadhi kumbukumbu za wastaafu kielektroniki, ili kurahisisha malipo kufanyika kwa wakati.

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nisisitize kwa maafisa utumishi wote wanaohusika kuandaa mapema nyaraka za watumishi wanaotarajia kustaafu na kuziwasilisha Hazina zikiwa zimekamilika ili malipo ya mafao, pensheni na mirathi ya wastaafu wa kawaida yafanyike kwa wakati na kuwaondolea adha ya usumbufu watumishi pindi wanapokuwa wamestaafu. Aidha, nahimiza ofisi zote za umma zitunze taarifa za

watumishi wa umma kielektroniki kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao.

### 4.1.16 Udhibiti wa Utakasishaji Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi

**153.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Wizara kupitia Kitengo cha Udhibiti wa Utakasishaji Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu ya Mwaka 2012 na Sheria ya Udhibiti Fedha Haramu na Mali Athirika ya Zanzibar ya Mwaka 2009 kwa kutekeleza yafuatayo: kufanya marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu (*The Anti-Money Laundering Act, 2006)* na kanuni zake za mwaka 2012 ili kuendana na mahitaji; kuendelea na utekelezaji wa mikakati ya kitaifa na kimataifa ya udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; kuendelea kupokea na kuchambua taarifa za miamala shuku zinazohusu utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi na taarifa za usafirishaji wa fedha kutoka na kuingia nchini kupitia mipakani; na kuendelea kuwasilisha taarifa za intelijensia kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria.

### 4.1.17 Tume ya Pamoja ya Fedha

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, pamoja na majukumu mengine Wizara kupitia Tume imepanga kutekeleza yafuatayo:- kufanya uchambuzi katika Usimamizi wa Deni la Serikali ili Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zishauriane katika kuimarisha Usimamizi wa Deni la Serikali; na kufanya uchambuzi wa Mapato na Matumizi yanayohusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano.

### 4.1.18 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Wizara itaendelea kufanya yafuatayo: kufanya marekebisho ya Sheria na Kanuni za Ubia ili kuimarisha usimamizi wa mifumo ya usimamiaji wa miradi ya ubia ikiwa ni pamoja na kupunguza mlolongo wa uidhinishaji wa miradi hiyo; kusimamia uibuaji na utekelezaji wa miradi ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP); kuandaa miongozo ya kitaalam ya kuainisha miradi; kufanya uchambuzi na uidhinishaji wa miradi ya PPP; na kutoa mafunzo na kuhamasisha kuhusu utekelezaji wa miradi ya ubia kwenye

Wizara, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma na taasisi binafsi.

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za utekelezaji inategemea kukamilisha maandiko ya ujenzi wa reli ya Mchuchuma/ Liganga – Mtwara kwa kiwango cha *standard gauge*; ujenzi wa reli ya Tanga – Arusha – Musoma kwa kiwango cha *standard gauge*; ujenzi wa miundombinu ya reli katika jiji la Dar Es Salaam kwa ajili ya treni ya abiria na mradi wa kusambaza gesi asilia nchini. Aidha, hatua ya kutangaza mradi wa ujenzi wa viwanda vya uzalishaji wa madawa muhimu na vifaa tiba chini ya MSD ili kuwapata wawekezaji itaendelea.

### 4.1.19 Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma

**157.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19, Wizara kupitia Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma itaendelea kuziwezesha Wizara, Idara Zinazojitegema, Wakala, Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutekeleza maboresho ya usimamizi wa fedha za umma. Programu hii inalenga kuboresha maeneo

mbalimbali yakiwemo: marekebisho ya sheria za kodi (Sheria ya Kodi ya Mapato, Sheria ya Ongezeko la Thamani, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na Sheria ya Ushuru wa Forodha) ili sheria hizi ziendane na Sheria ya Uwekezaji; kuhuisha mikataba ya madini ambayo inapata misamaha ya kodi; na kuhuisha mfumo wa kufanya maoteo ya viashiria vya uchumi jumla.

**158.** ***Mheshimiwa Spika***, maeneo mengine ya maboresho ni pamoja na: kuandaa na kukamilisha Sera ya Kitaifa ya Ufuatiliaji na Tathmini; kuhuisha mikataba ya makubaliano na Mashirika ya Maendeleo ili iendane na Sheria za Kodi za Tanzania; kufanya tathmini ya matokeo ya kiutendaji ya mfumo wa vihatarishi katika Wizara, Taasisi, Wakala na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani; kuanzisha Ofisi mpya za Mhakiki Mali wa Serikali katika mikoa ya Simiyu, Katavi na Songwe; kufanya marekebisho ya sheria ya Udalali ya mwaka 1928; na kuimarisha ununuzi wa Umma kwa kuzingatia thamani ya fedha, kuweka udhibiti na usimamizi.

### 4.1.20 Mradi wa Kimkakati wa kuongeza mapato kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa (Strategic Revenue Generation in LGAs Project)

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Mradi huu, Wizara itatoa fedha katika Serikali za Mitaa zitakazokidhi vigezo vya miradi ya kimkakati ya kuongeza mapato ya Serikali za Mitaa. Aidha, Wizara imepanga kutoa mafunzo kwa wawezeshaji wa kitaifa juu ya Usimamiaji na Uandaaji wa Miradi ya Kimkakati ya kuongeza mapato kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

## 4.2 USIMAMIZI NA URATIBU WA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA CHINI YA WIZARA

### 4.2.1 Huduma za kibenki

**(i) Benki Kuu ya Tanzania (BOT)**

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Benki Kuu ya Tanzania imepanga kutekeleza yafuatayo: kuendelea kutekeleza sera ya fedha yenye kuongeza ukwasi katika uchumi ili kuendeleza ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na

shughuli mbalimbali za uchumi bila kuchochea mfumuko wa bei; kuendelea kuhakikisha kuwa kunakuwepo na ufanisi katika masoko ya fedha ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa utulivu wa viwango vya riba kama chachu ya kuongeza upatikanaji wa mikopo nafuu kwa sekta binafsi; na kutumia mfumo mpya wa kutekeleza sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu (Central Bank Policy Rate) katika kutoa mwelekeo wa sera ya fedha badala ya kutumia fedha taslimu. Riba hii itakuwa ikitoa muongozo wa sera ya fedha unaoendana na malengo mapana ya Serikali ya kudhibiti mfumuko wa bei na kukuza uchumi.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni matarajio ya Wizara kuwa mfumo huu mpya utakapoanza kufanya kazi utaboresha viwango vya riba kwenye taasisi zetu za fedha pamoja na masoko yetu ya fedha, na kupelekea riba za mikopo kuwa katika viwango vinavyoendana na hali halisi ya uchumi na mahitaji yake.

### (ii) Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB)

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Benki ya Maendeleo ya Kilimo itatekeleza yafuatayo: Kutoa mikopo kwa ajili ya miradi ya

umwagiliaji, miradi ya mfumo wa nyukliasi (nucleus farms), miradi ya maghala, na kuanzisha vituo vya huduma na zana za kilimo (farm clinics and mechanization centers); kuendelea kutekeleza mpango wa kuwajengea uwezo wakulima wadogo wadogo kupitia mafunzo ya usimamizi wa fedha, oganaizesheni ya vikundi na vyama, utunzaji wa kumbukumbu na utengenezaji wa miradi inayokidhi masharti ya mikopo kutoka katika benki na taasisi za fedha na kukamilisha zoezi la ufunguzi wa ofisi ya Benki Dodoma na Ofisi ya TADB Kanda ya Ziwa jijini Mwanza.

### (iii) Benki ya Maendeleo TIB (TIB DFI)

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Benki ya Maendeleo ya TIB imepanga kutekeleza yafuatayo: kuendelea kutoa mikopo ya muda mrefu na ya kati kwa wajasiriamali; kuendeleza maeneo ya viwanda kwa wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kushirikiana na SIDO na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA); na kukuza biashara na kuongeza ushiriki wa wananchi kwenye upembuzi wa miradi na ukopeshaji kwa viwanda vya kuchakata mazao na malighafi. Aidha, Benki pia imepanga kutoa mikopo ya thamani ya shilingi bilioni 688.29 na Waraka

Mizania wa benki unatarajiwa kukua kutoka shilingi bilioni 757.06 mwaka 2017 hadi kufikia shilingi bilioni 864.94 mwaka 2018 ikiwa ni ongezeko la asilimia 14.

**(iv) Benki ya Biashara TIB (TIB CBL)**

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Benki kwa kushirikiana na kampuni mama ya TIB DFI, imepanga kutoa mikopo ya shilingi bilioni 40 kwa kampuni na Taasisi zinazofanya vizuri katika biashara ya pamba, kutoa mikopo ya shilingi bilioni 20 kwa miradi mbalimbali na kutoa barua na dhamana za mikopo ya thamani ya shilingi bilioni 15.

**(v) Benki ya TPB**

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2018, Benki ya TPB imeweka lengo la kukuza amana za wateja hadi kufikia shilingi bilioni 422 na kutoa mikopo ya shilingi bilioni 389. Aidha, benki inatarajia kuongeza mapato kutoka shilingi bilioni 107.96 mwaka 2017 hadi kufikia shilingi bilioni 121.47 mwaka 2018.

### 4.2.2 Rufani za Kodi

**166.** ***Mhesimiwa Spika,*** kwa mwaka 2018/19, Bodi ya Rufani za Kodi (TRAB) kwa kushirikiana na Baraza la Rufani za Kodi (TRAT) zitaendelea kusikiliza na kutolea maamuzi rufaa za kodi kwa haraka na ueledi ili kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati, kutoa elimu ya sheria za kodi na utatuzi wa migogoro ya kodi kwa Wenyeviti na Wajumbe wapya wa Bodi, kutoa elimu kwa wadau wa kodi juu ya taratibu za kukata rufaa za kodi na kuchapisha ripoti za maamuzi ya kodi yaani "Tanzania Tax Law Reports" zinazojumuisha maamuzi yaliyotolewa mwaka 2013-14 kwa ajili ya rejea kwa wadau wa kodi. Aidha,ili kuongeza kasi ya kusikiliza na kutoa maamuzi ya rufaa za kodi, Bodi imepanga kuanzisha vikao maalum vya kusikiliza mashauri ya rufani.

### 4.2.3 Huduma za Bima

#### (i) Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima (TIRA)

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Mamlaka imepanga kutekeleza yafuatayo: kukamilisha Sera ya Taifa ya Bima na kanuni za

ukuzaji na usimamiaji wa soko la bima ili kuongeza mapato; kuwekeza katika miundombinu na mifumo ya kielektroniki ili kurahisisha biashara ya bima na udhibiti; kujenga uwezo wa wataalam wa bima nchini na wafanyakazi wa Mamlaka katika usimamizi wa kanuni mbalimbali za Bima; kupata hati ya viwango vya kimataifa (ISO) na kuendeleza kukuza sekta ya Bima ili iweze kukuza mchango wake kwenye Pato la Taifa.

**(ii) Shirika la Bima la Taifa (NIC)**

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Shirika la Bima litatekeleza yafuatayo: kuanzisha bima ya kilimo; kufuatilia biashara ya bima kwa taasisi za Serikali ambazo hazijanunua bima kutoka Shirika la Bima la Taifa; kuanzisha mfumo mpya wa kidijitali wa bima za COMESA utakaookomesha bima za bandia. Aidha, shirika linatarajia kukusanya mapato ya shilingi bilioni 99.79.

### 4.2.4 Mitaji na Dhamana

**(i) Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)**

**169.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/19, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imepanga kufanya yafuatayo: kukamilisha sheria mpya ya Masoko ya Mitaji; kukamilisha Mpango Mkuu wa Kitaifa wa Maendeleo ya Masoko ya Mitaji; kuongeza idadi na bidhaa katika Soko la Hisa; kuimarisha udhibiti wa masoko kwa kukamilisha uanzishwaji wa misingi ya kusimamia masoko kwa kuzingatia uzito wa athari (risk based supervision); kutoa elimu kwa umma na kuhamasisha Mamlaka ya Serikali za mitaa kutumia Masoko ya Mitaji kupata fedha kwa kutumia Hatifungani za Serikali za Mitaa kwa miradi ya maendeleo ambayo inaweza kujiendesha yenyewe.

**(ii) Soko la Bidhaa Tanzania – Tanzania Commodity Exchange Market**

**170. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2018/19 Soko la Bidhaa limepanga kufanya yafuatayo:

kuendelea kukusanya mtaji wa Soko la Bidhaa kutoka Sekta ya Umma na Binafsi; kuendelea kushawishi vyama vya ushirika na wafanyabiashara wa mazao kuanzisha kampuni za kutoa huduma za uwakala kwenye soko la bidhaa; kupitia mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo na kuandaa mpango wa uhusishaji wadau; na kukamilisha ununuzi na kufunga mfumo wa kielektroniki wa mauzo, uhawilishaji bidhaa na malipo, utoaji wa taarifa za masoko ili kuliwezesha Soko kuendeshwa kisasa. Aidha, Soko limepanga kutumia Balozi za Tanzania nje ya nchi kutafuta masoko na kuongeza wanunuzi wa mazao kupitia Soko la Bidhaa; kushirikiana na Idara ya Habari Maelezo, Bodi ya Stakabadhi za Ghala na wadau wengine katika kutoa elimu kwa umma kwa njia ya runinga na redio kuhusu Mfumo wa Stakabadhi Ghalani na Soko la Bidhaa; kutembelea maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na biashara ili kutoa elimu na kuwahimiza wakulima kuongeza mazao zaidi kwenye mfumo wa Stakabadhi za Ghala na kuwezesha mazao hayo kuuzwa kwenye Soko la Bidhaa.

### (iii) Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE)

**171.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2018/19; Soko la Hisa Dar Es Salaam linalenga kufanya yafuatayo: kuimarisha muundo na usimamizi wa uendeshaji wa soko pamoja na Kampuni yake Tanzu ya CSD & Registry Company Ltd; kutekeleza mpango wa kuanzisha Hatifungani za rejareja za Serikali Kuu (Micro-Savings products, M-Akiba Bonds) na Hatifungani za Serikali za Mitaa; kuongeza kiwango cha ukwasi sokoni kwa kuboresha kanuni za uuzaji na ununuzi wa dhamana; kuimarisha miundo mbinu ya mauzo ya dhamana; na kuimarisha muonekano wa Soko la Hisa kwa wawekezaji wa ndani na nje.

**172.** ***Mheshimiwa Spika***, Soko la Hisa la Dar Es Salaam litaendelea kuongeza idadi ya kampuni zitakazoorodheshwa sokoni kufikia 32 na kuanzisha bidhaa na huduma mpya sokoni kama *Negotiable Certificate of Deposits (NCDs), Closed-Ended Investment Funds (CIS),* pamoja na *Real Estate Investments Trusts (REITs)*; na kupata Uanachama wa Kudumu katika Shirikisho la Masoko ya Hisa Duniani.

#### 4.2.5 Dhamana za Uwekezaji Tanzania

**(i) Taasisi ya Huduma za Fedha na Mikopo Tanzania (UTT MFI)**

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Taasisi inatarajia Kutoa mikopo yenye thamani jumla ya shilingi bilioni 22 kwa wafanyakazi wa Umma, wafanyabiashara na wakulima wapatao 9,000; kuendelea kufuatilia marejesho ya mikopo chechefu; kuendelea kutoa huduma za wakala wa uuzaji wa vipande vya UTT AMIS, Wakala wa huduma za kibenki (Benki ya CRDB) na Wakala wa Bima.

**(ii) Kampuni ya Usimamizi wa Rasilimali za Uwekezaji (UTT AMIS)**

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2018/19, Kampuni imepanga kufanya yafuatayo: kuongeza rasilimali za mfuko kwa asilimia 15; kuongeza idadi ya wawekezaji kwa asilimia 5 ili wanufaike na fursa za uwekezaji zilizopo nchini kupitia mifuko ya UTT AMIS; kutoa viwango shindani vya faida kwa wawekezaji kwenye mifuko ya uwekezaji wa pamoja na huduma za usimamizi mitaji binafsi;

kuzihusisha zaidi Taasisi za Serikali, Mifuko ya Hifadhi za Jamii, Mashirika na vikundi mbalimbali vya kijamii kama vile SACCOS ili zijiunge na mifuko ya UTT AMIS kwa lengo la kukuza mitaji yao.

**(iii) Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu (UTT PID)**

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, UTT PID inatarajia kutekeleza yafuatayo:- uendelezaji wa viwanja vya balozi mbalimbali za Tanzania zilizopo nchi za nje (Abuja Nigeria na Lusaka Zambia); usimamizi wa majengo; uuzaji wa viwanja; na ushauri wa mambo ya kibiashara na miradi. Aidha, Taasisi itaendelea kuboresha utayarishaji wa upembuzi yakinifu katika miradi yake na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

### 4.2.6 Taasisi za Mafunzo

**(i) Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM)**

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19 Chuo cha Usimamizi wa Fedha kinatarajia kufanya yafuatayo: kudahili wanafunzi 9,200 katika fani

mbalimbali; kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri elekezi; kuendeleza kampasi mpya ya Msata na Mwanza; na kukamilisha umiliki wa eneo la upanuzi wa Chuo katika Jiji la Dodoma (ekari 769).

### (ii) Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP)

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Chuo kitaendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na: kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 5,784 hadi kufikia wanafunzi 7,000; kuboresha miundombinu ikiwa ni pamoja na kuanza kujenga jengo la tatu la mafunzo katika Kituo cha Kanda ya Ziwa Mwanza; kuanza ujenzi wa Bweni la wasichana lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 192 katika Kampasi ya Dodoma; kuajiri watumishi wapya 90; na kuongeza uwezo wa kiutendaji kwa watumishi 226.

### (iii) Taasisi ya Uhasibu Arusha (IAA)

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Taasisi inatarajia kutekeleza yafuatayo: kudahili

wanafunzi 4,000 kutoka 3,849 waliopo sasa; kutafuta mwekezaji kwa utaratibu wa PPP ili kupata madarasa, kumbi za mikutano na mabweni; kuandaa kongamano la nane la Kimataifa la ununuzi kwa kushirikiana na PPRA na kufanya utafiti kwa kushirikiana na Coventry University cha Uingereza katika eneo la mafuta na gesi na maeneo mengine.

**(iv) Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA)**

**179.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2018/19, Taasisi imepanga kusimammia utoaji wa elimu bora kwa: kuajiri wahadhiri wenye sifa; kuboresha huduma za maktaba na huduma ya mtandao kwenye kampasi zote; kudhamini wahadhiri wanaojiunga na kozi za Uzamili na Uzamivu; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ili kuwezesha kuongeza udahili wa wanafunzi na kuboresha mazingira ya kujifunza.

**(v) Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC)**

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, chuo kimepanga kuendelea kutoa na kuboresha

huduma na mafunzo ya Takwimu rasmi na takwimu za kilimo; kuongeza udahili wa wanafunzi katika ngazi zote za programu; kuwajengea uwezo wanataaluma kwa kuwapa mafunzo ya kivitendo katika maeneo ya mifumo ya uchakataji wa takwimu; kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi; kuendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia; kupitia upya mitaala ya programu za Chuo; kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani ya takwimu rasmi kwa watumishi wa ofisi za Taifa za Takwimu kutoka katika nchi 18 zinazotumia lugha ya kiingereza barani Afrika; kuendelea kuzisaidia Wizara, Idara za Serikali, Mashirika ya Umma na kampuni binafsi katika kujenga mifumo bora ya ukusanyaji na uchambuzi wa Takwimu ili kuhamasisha matumizi ya takwimu rasmi; na kuanzisha utoaji mafunzo kwa njia ya masafa.

### 4.2.7 Taasisi za kitaalam na Huduma nyinginezo

#### (i) Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatarajia

kukusanya jumla ya shilingi bilioni 18,000.22 sawa na ongezeko la asilimia 5 ikilinganishwa na matarajio ya makusanyo ya mwaka 2017/18. Ili kufikia lengo hilo, Mamlaka imeweka mikakati ifuatayo: kusajili walipakodi wapya na kuhakikisha walipakodi wote waliosajiliwa wanalipa kodi kwa mujibu wa sheria; kufanya tafiti kwa ajili ya kuibua vyanzo vipya vya kodi na fursa zilizopo ili kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato; kuwezesha mifumo ya kodi kutambua malipo kwa kutumia huduma za simu za mkononi; kuanza kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Stempu za Kodi kwenye viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa na zile zinazoingizwa nchini; na kuboresha na kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa kutolea risiti za kodi (EFDMS) ili kuwezesha ufuatiliaji wa karibu wa mauzo na utoaji wa risiti kwa kila ununuzi badala ya kutumia risiti za makundi.

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** mikakati mingine itakayotekelezwa ni pamoja na: kuendelea na utekelezaji wa zoezi la kuwapatia vitambulisho maalum wafanyabiashara wadogo walio kwenye sekta isiyo rasmi kwa mikoa yote nchini; kutekeleza mradi wa dirisha moja la Forodha ili kuwaweka pamoja wadau wote wa kuondosha

mizigo bandarini na mipakani; na kufunga mashine za mionzi bandarini, viwanja vya ndege na mipaka mikubwa; kuunganisha taarifa za majengo zilizoko katika mfumo wa kodi ya majengo, taarifa za uhakiki wa majengo na ramani za satelaiti zilizo katika kanzidata ya *Geographical Information System - GIS* katika Halmashauri mbalimbali nchini ili kurahisha ukusanyaji wa kodi ya majengo; na kuunganisha mifumo ya kutolea taarifa za miamala ya michezo ya kubahatisha inayofanywa kwenye nyumba za kamari na mifumo ya kukusanyia kodi iliyoko Mamlaka ya Mapato.

### (ii) Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imepanga kutayarisha na kutoa takwimu rasmi kwa wakati; kufanya maandalizi ya Sensa ya Idadi ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022; na Kufanya Maandalizi ya Mpango Kabambe wa Pili wa Kitaifa wa Kuimarisha na Kuboresha Takwimu Tanzania (TSMP) kwa kipindi cha 2018/19 - 2023/24.

### (iii) Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA)

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2018/19, Bodi imepanga kutekeleza yafuatayo: kusajili watahiniwa, wanachama na kampuni za uhasibu na ukaguzi; kufanya ukaguzi na kusimamia ubora wa kazi za ukaguzi; kutoa miongozo ya viwango vya uhasibu na ukaguzi; kutoa mafunzo endelevu kwa wanataaluma na wadau wengine; kutoa huduma ya ushauri elekezi na ufundi; kujenga uwezo wa rasilimali watu; kusimamia uanzishaji wa mitaala mipya katika kuendesha mitihani ya uhasibu; kukamilisha muundo wa mifumo ya uwekaji kumbukumbu na mawasiliano; na kuendelea kushirikiana na Taasisi nyingine kama TRA, BRELA na BoT katika kuwaelimisha wadau kuweza kuelewa na kutumia viwango vya uhasibu na ukaguzi vinavyokubalika.

### (iv) Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (Gaming Board)

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19, Bodi imepanga kuendelea kusimamia vyema uendeshaji wa sekta ya michezo ya kubahatisha

nchini na kuhakikisha kwamba inaendelea kuendeshwa kwa mujibu wa sheria na taratibu. Aidha, Bodi itaanzisha mfumo wa kielektroniki wa *Regulator Central Monitoring System (RCEMS).* Mfumo huu unatarajia kuunganisha mifumo ya uendeshaji wa michezo ya *Sports betting* kwa lengo la kurahisisha ukusanyaji wa taarifa mbalimbali za fedha itokanayo na uendeshaji wa michezo hiyo.

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi itaendelea kuweka msisitizo katika dhana ya "responsible gaming" ili ushiriki wa jamii yetu katika michezo hii iwe ni kwa ajili ya burudani na sio chanzo kikuu cha mapato. Vilevile, Sheria inayokataza ushiriki wa watoto itaendelea kusimamiwa kwa makini zaidi na Bodi itachukua hatua kali sana kwa waendeshaji watakaothubutu kukiuka.

### (v) Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha (SELF Microfinance Fund)

**187.** ***Mheshimiwa Spika***; kwa mwaka 2018/19, Mfuko umepanga kutekeleza yafuatayo: kuimarisha mifumo ya Mfuko; kutoa mikopo ya thamani ya shilingi bilioni 25.0 kwa kiwango cha urejeshaji

kufikia angalau asilimia 95; kutoa mafunzo kwa viongozi na watendaji wa asasi zipatazo 160 na mafunzo ya ujasiriamali kwa walengwa wapatao 2,000; kutoa mikopo kwa ajili ya kuimarisha uchumi wa viwanda vya usindikaji wa mafuta ya alizeti mkoa wa Singida na mvinyo wa zabibu mkoa wa Dodoma; na kutafuta vyanzo zaidi vya fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo na kujenga ushirikiano katika nyanja mbalimbali zikiwemo kujenga uwezo wa Asasi na Wajasiriamali wadogo.

## 5.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/19

### 5.1 MAKADIRIO YA MAPATO

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2018/19 Wizara inakadiria kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi bilioni 597.81 kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na mauzo ya nyaraka za zabuni, kodi za pango, mauzo ya leseni za udalali, gawio, marejesho ya mikopo na michango kutoka katika Taasisi na Mashirika ya Umma.

## 5.2 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2018/19

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Fedha na Mipango imepanga kutumia kiasi cha jumla ya **shilingi 12,058,714,013,500 (Bilioni 12,058.71)** kwa mafungu yote nane. Kati ya fedha hizo, shilingi **10,763,501,474,000 (Bilioni 10,763.50)** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 1,295,212,539,500 (Bilioni 1,295.21)** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Matumizi ya Kawaida yanajumuisha **shilingi 65,764,075,000 (Bilioni 65.76)** kwa ajili ya mishahara, **shilingi 693,257,399,000 (Bilioni 693.26)** kwa ajili ya matumizi Mengineyo (OC) na shilingi **10,004,480,000,000 (Bilioni 10,004.48)** ni malipo ya deni la Serikali na michango ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Aidha, katika fedha za matumizi ya maendeleo, **shilingi 1,266,033,128,500 (Bilioni 1,266.03)** ni fedha za ndani na **shilingi 29,179,411,000 (Bilioni 29.18)** ni fedha za nje.

## MAOMBI YA FEDHA

### 5.2.1 FUNGU 50 – WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika fungu hili kwa mwaka 2018/19, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

**(a)** Matumizi ya kawaida - **Shilingi 57,022,927,000 (bilioni 57.02).** Kati ya hizo:

(i) Mishahara - **Shilingi 7,577,332,000 (bilioni 7.58)**

(ii) Matumizi mengineyo – **Shilingi 49,445,595,000 (bilioni 49.44)**

**(b)** Miradi ya Maendeleo - **Shilingi 28,790,817,000 (bilioni 28.79).** Kati ya hizo:

(i) Fedha za Ndani - **Shilingi 19,642,535,000 (bilioni 19.64).**

(ii) Fedha za Nje - **Shilingi 9,148,282,000 (bilioni 9.15).**

### 5.2.2 FUNGU 21 - HAZINA

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Fungu hili kwa mwaka 2018/19, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

**(a)** Matumizi ya Kawaida – **Shilingi 531,890,056,000 (bilioni 531.89)**. Kati ya fedha hizo:

(i) Mishahara ya fungu hili - **Shilingi 21,467,017,000 (bilioni 21.47)**.

(ii) Matumizi Mengineyo – **Shilingi 510,423,039,000.00 (bilioni 510.42)** ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya idara, taasisi zilizo chini ya Fungu hili, pamoja na matumizi maalum.

**(b)** Miradi ya Maendeleo – **Shilingi 1,247,611,267,500 (bilioni 1,247.61).** Kati ya hizo:

(i) Fedha za Ndani - **Shilingi 1,236,190,593,500 (bilioni 1,236.19)**

(ii) Fedha za Nje - **Shilingi 11,420,674,000 (bilioni 11.42)**

### 5.2.3 FUNGU 22- DENI LA TAIFA

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika fungu hili kwa mwaka 2018/19, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

**(a)** Matumizi ya kawaida – **Shilingi 10,013,706,140,000** (**bilioni 10,013.71**). Kati ya fedha hizo:

(i) Mishahara - **Shilingi 9,226,140,000 (bilioni 9.23)**

(ii) Matumizi Mengineyo (Malipo ya Madeni na Michango ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii) – **Shilingi 10,004,480,000,000 (bilioni 10,004.48)**

### 5.2.4 FUNGU 23 – MHASIBU MKUU WA SERIKALI

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Fungu hili kwa mwaka 2018/19, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

**(a)** Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 46,725,409,000 (bilioni 46.72).** Kati ya fedha hizo:

(i) Mishahara – **Shilingi 7,908,675,000 (bilioni 7.91)**

(ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi Shilingi 38,816,734,000 (bilioni 38.82)**

**(b)** Miradi ya Maendeleo **– Shilingi 3,200,000,000.00 (bilioni 3.20).** Kati ya fedha hizo:

(i) Fedha za Ndani - **Shilingi 2,000,000,000.00 (bilioni 2.00).**

(ii) Fedha za Nje - **Shilingi 1,200,000,000.00 (bilioni 1.20).**

### 5.2.5 FUNGU 7 – OFISI YA MSAJILI WA HAZINA

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Fungu hili kwa mwaka 2018/19, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

**(a)** Matumizi ya kawaida – **Shilingi 54,592,065,000.00 (bilioni 54.59).** Kati ya fedha hizo:-

(i) Mishahara - **Shilingi 2,362,279,000.00 (bilioni 2.36)**

(ii) Matumizi Mengineyo- **Shilingi Shilingi 52,229,786,000.00 (bilioni 52.23).**

**(b)** Miradi ya Maendeleo **– Shilingi 1,650,000,000.00 (bilioni 1.65).** Kati ya fedha hizo:

(i) Fedha za Ndani – **Shilingi 1,000,000,000.00 (bilioni 1).**

(ii) Fedha za Nje -**Shilingi 650,000,000.00 (bilioni 0.65).**

### 5.2.6 FUNGU 10 – TUME YA PAMOJA YA FEDHA

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Fungu hili kwa mwaka 2018/19, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Kawaida - **Shilingi 2,155,075,000 (bilioni 2.15).** Kati ya fedha hizo:-

(i) Mishahara - **Shilingi 574,933,000 (bilioni 0.57)**

(ii) Matumizi Mengineyo- **Shilingi 1,580,142,000 (bilioni 1.58).**

### 5.2.7 FUNGU 13 – KITENGO CHA KUDHIBITI FEDHA HARAMU

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Fungu hili kwa mwaka 2018/19, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida - **Shilingi 2,015,586,000 (bilioni 2.01).**

(b) Miradi ya Maendeleo **– Shilingi 248,363,000 (bilioni 0.25)** ambazo ni fedha za nje.

### 5.2.8 FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Fungu hili kwa mwaka 2018/19, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:

(a) Matumizi ya kawaida – **Shilingi 55,394,216,000 (bilioni 55.39).** Kati ya fedha hizo:

(i) Mishahara - **Shilingi 16,647,699,000 (bilioni 16.65).**

(ii) Matumizi Mengineyo - **Shilingi 38,746,517,000 (bilioni 38.75).**

(b) Miradi ya Maendeleo **– Shilingi 13,712,092,000 (bilioni 13.71).** Kati ya fedha hizo:

(i) Fedha za Ndani – **Shilingi 7,200,000,000 (bilioni 7.20).**

(ii) Fedha za Nje -**Shilingi 6,512,092,000 (bilioni 6.51).**

## 6.0 SHUKRANI

**198.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba nitumie fursa hii kuzishukuru nchi na mashirika mbalimbali ya kimataifa ambayo kwa namna moja ama nyingine yamesaidia katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara. Aidha, napenda kuwashukuru sana Wafanyakazi na wananchi wote ambao wameendelea kulipa kodi kwa hiari na pia kushiriki katika ujenzi wa Taifa letu.

**199.** ***Mheshimiwa Spika***, mwisho kabisa napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara (www.mof.go.tz).

**200.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

## 7.0 VIAMBATISHO

**Jedwali Na.1: Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango**

| Na: | Taasisi/ Shirika |
|---|---|
| 1 | Ofisi ya Msajili wa Hazina -TRO |
| 2 | Benki Kuu ya Tanzania - BOT |
| 3 | Mamlaka ya Mapato Tanzania - TRA |
| 4 | Mfuko wa Pensheni wa PSPF |
| 5 | Mfuko wa Pensheni wa GEPF |
| 6 | Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma - PPRA |
| 7 | Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima - TIRA |
| 8 | Mfuko wa Pensheni wa PPF |
| 9 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania - TIA |
| 10 | Chuo cha Usimamizi wa Fedha - IFM |
| 11 | Chuo cha Uhasibu Arusha - IAA |
| 12 | Chuo cha Takwimu cha Afrika Mashariki – EASTC |
| 13 | Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini - IRDP |
| 14 | Kitengo cha Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu - FIU |
| 15 | Ofisi ya Taifa ya Takwimu - NBS |
| 16 | Mamlaka ya Rufaa za Zabuni - PPAA |
| 17 | Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini - GPSA |
| 18 | Tume ya Pamoja ya Fedha - JFC |
| 19 | Taasisi ya Miradi na Maendeleo ya Miundombinu - UTT-PID |
| 20 | Taasisi ya Huduma za fedha na Mikopo - UTT-MFI |
| 21 | Taasisi ya Huduma za Uwekezaji wa Pamoja - UTT-AMIS |
| 22 | Bodi ya Michezo ya Kubahatisha - GBT |

| Na: | Taasisi/ Shirika |
|---|---|
| 23 | Benki ya Maendeleo ya TIB -TIB DFI |
| 24 | Benki ya TIB Corporate –TIB CFL |
| 25 | Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania - TADB |
| 26 | Mamlaka ya Masoko ya Mitaji ya Dhamana - CMSA |
| 27 | Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha (SELF Microfinance Fund) |
| 28 | Bodi ya Wataalamu Ununuzi na Ugavi - PSPTB |
| 29 | Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Ukaguzi - NBAA |
| 30 | Benki ya TPB |
| 31 | Benki ya Twiga – Twiga Bancorp LTD |
| 32 | Shirika la Bima la Taifa – NIC |
| 33 | Baraza la Rufani za Kodi – TRAT |
| 34 | Bodi ya Rufani za Kodi – TRAB |
| 35 | Soko la Hisa la Dar es Salaam – DSE |
| 36 | Soko la Bidhaa Tanzania – TMX |

**Jedwali Na. 2 : Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida mwaka 2017/18**

***Shilling***

| Fungu | Fedha zilizoidhinishwa 2017/2018 | Matumizi hadi Aprili 2018 | Asilimia ya matumizi |
|---|---|---|---|
| **FUNGU 50 - WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO** | | | |
| Mishahara | 8,077,009,000 | 5,619,890,272 | 70 |
| Matumizi Mengineyo | 46,962,634,000 | 38,375,366,439 | 82 |
| **Jumla Fungu 50** | **55,039,643,000** | **43,995,256,711** | **80** |
| **FUNGU 23 - IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI** | | | |
| Mishahara | 8,404,104,000 | 5,354,876,020 | 64 |
| Matumizi Mengineyo | 37,556,734,000 | 32,044,498,736 | 85 |
| **Jumla Fungu 23** | **45,960,838,000** | **37,399,374,756** | **81** |
| **FUNGU 22-DENI LA TAIFA** | | | |
| Mishahara | 10,689,300,000 | 4,967,187,856 | 46 |
| Matumizi Mengineyo | 9,461,433,000,000 | 7,939,143,764,571 | 84 |
| **Jumla Fungu 22** | **9,472,122,300,000** | **7,944,110,952,426** | **84** |
| **FUNGU 21- HAZINA** | | | |
| Mishahara | 40,643,601,000 | 3,587,380,992 | 9 |
| Matumizi Mengineyo | 529,785,647,000 | 447,739,900,105 | 85 |
| **Jumla Fungu 21** | **570,429,248,000** | **451,327,281,096** | **79** |

| Fungu | Fedha zilizoidhinishwa 2017/2018 | Matumizi hadi Aprili 2018 | Asilimia ya matumizi |
|---|---|---|---|
| **FUNGU 13 - KITENGO CHA KUDHIBITI FEDHA HARAMU** | | | |
| Mishahara | - | - | |
| Matumizi Mengineyo | 1,515,586,000 | 1,086,313,887 | 72 |
| **Jumla Fungu 23** | **1,515,586,000** | **1,086,313,887** | **72** |
| **FUNGU 10 - TUME YA PAMOJA YA FEDHA** | | | |
| Mishahara | 428,676,000 | 294,535,612 | 69 |
| Matumizi Mengineyo | 958,141,511 | 722,830,000 | 75 |
| **Jumla Fungu 10** | **1,386,817,511** | **1,017,365,612** | **73** |
| **FUNGU 7-OFISI YA MSAJILI WA HAZINA** | | | |
| Mishahara | 2,687,702,000 | 1,720,149,261 | 64 |
| Matumizi Mengineyo | 102,229,786,000 | 8,711,856,661 | 9 |
| **Jumla Fungu 7** | **104,917,488,000** | **10,432,005,922** | **10** |
| **FUNGU 45-OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI** | | | |
| Mishahara | 17,313,756,068 | 11,345,093,136 | 66 |
| Matumizi Mengineyo | 44,519,191,932 | 37,579,150,540 | 84 |
| **Jumla Fungu 45** | **61,832,948,000** | **48,924,243,676** | **79** |
| **FUNGU 66 -TUME YA MIPANGO** | | | |
| Mishahara | 1,603,212,000 | 991,213,500 | 62 |
| Matumizi Mengineyo | 3,333,152,000 | 2,735,739,947 | 82 |

| Fungu | Fedha zilizoidhinishwa 2017/2018 | Matumizi hadi Aprili 2018 | Asilimia ya matumizi |
|---|---|---|---|
| **Jumla Fungu 66** | **4,936,364,000** | **3,726,953,447** | **75** |
| **MUHTASARI WA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MAFUNGU YOTE** | | | |
| Jumla Ndogo - Mishahara | 89,847,360,068 | 33,880,326,649 | 38 |
| Jumla Ndogo-Matumizi Mengineyo | 10,228,293,872,443 | 8,508,139,420,885 | 83 |
| **JUMLA KUU** | **10,318,141,232,511** | **8,542,019,747,534** | **83** |

***Chanzo**: Wizara ya Fedha na Mipango, Mei, 2018*

**Jedwali Na.3: Mchanganuo wa Matumizi ya Fedha za Maendeleo mwaka 2017/18**

***Shilingi***

| Fungu | Fedha zilizoidhinishwa 2017/2018 | Matumizi hadi Aprili 2018 | Asilimia ya Matumizi |
|---|---|---|---|
| **FUNGU 50 - WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO** | | | |
| Fedha za Ndani | 3,500,000,000 | - | 0 |
| Fedha za Nje | 8,070,500,000 | 4,284,005,592 | 53 |
| **Jumla Fungu 50** | **11,570,500,000** | **4,284,005,592** | **37** |
| **FUNGU 23 - IDARA YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI** | | | |
| Fedha za Ndani | 2,000,000,000 | 711,158,960 | 36 |

| Fungu | Fedha zilizoidhinishwa 2017/2018 | Matumizi hadi Aprili 2018 | Asilimia ya Matumizi |
|---|---|---|---|
| Fedha za Nje | 1,600,000,000 | 1,081,041,308 | 68 |
| **Jumla Fungu 23** | **3,600,000,000** | **1,792,200,268** | **50** |
| **FUNGU 21- HAZINA** | | | |
| Fedha za Ndani | 1,364,000,000,000 | 51,500,000,000 | 4 |
| Fedha za Nje | 31,636,701,741 | 21,651,677,097 | 68 |
| **Jumla Fungu 21** | **1,395,636,701,741** | **73,151,677,097** | **5** |
| **FUNGU 7-OFISI YA MSAJILI WA HAZINA** | | | |
| Fedha za Ndani | 1,000,000,000 | - | 0 |
| Fedha za Nje | 1,000,000,000 | 382,074,000 | 38 |
| **Jumla Fungu 7** | **2,000,000,000** | **382,074,000** | **19** |
| **FUNGU 45-OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI** | | | |
| Fedha za Ndani | 8,000,000,000 | 528,789,347 | 7 |
| Fedha za Nje | 3,800,948,000 | 376,135,033 | 10 |
| **Jumla Fungu 45** | **11,800,948,000** | **904,924,380** | **8** |
| **FUNGU 66 -TUME YA MIPANGO** | | | |
| Fedha za Ndani | 4,475,800,000 | 741,930,000 | 17 |
| Fedha za Nje | - | - | 0 |
| **Jumla Fungu 66** | **4,475,800,000** | **741,930,000** | **17** |
| **MUHTASARI WA MATUMIZI YA MAENDELEO KWA MAFUNGU YOTE** | | | |
| Jumla Ndogo-Fedha | 1,382,975,800,000.00 | 53,481,878,307.00 | |

| Fungu | Fedha zilizoidhinishwa 2017/2018 | Matumizi hadi Aprili 2018 | Asilimia ya Matumizi |
|---|---|---|---|
| za Ndani | | | 4 |
| Jumla Ndogo-Fedha za nje | 46,108,149,741 | 27,774,933,029 | 60 |
| **JUMLA KUU** | **1,429,083,949,741** | **81,256,811,336** | **6** |

***Chanzo**: Wizara ya Fedha na Mipango, Mei, 2018*

## JEDWALI NA 4: MALENGO NA MAKUSANYO HALISI

## KATIKA KIPINDI CHA MWEZI JULAI 2017 – APRILI 2018

***(TANZANIA BARA)*** ***Shilingi Milioni***

| Idara | 2016/17 | 2017/18 | | | Asilimia ya Ukuaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | Makusanyo | Lengo | Makusanyo | Ufanisi (%) | |
| Kodi za Ndani | 2,374,498.90 | 2,916,085.20 | 2,658,461.80 | 91.17 | 11.96 |
| Walipakodi Wakubwa | 4,579,990.70 | 5,497,408.90 | 4,904,919.10 | 89.22 | 7.09 |
| Ushuru wa Forodha | 4,785,478.00 | 5,990,903.70 | 5,082,991.60 | 84.85 | 6.22 |
| **Jumla (Ghafi)** | **11,739,967.60** | **14,404,397.80** | **.2,646,372.50** | **87.80** | **7.72** |
| Toa:Marejesho na Uhawilisho | 95,289.23 | 178,962.07 | 43,360.21 | 24.23 | -54.50 |
| **Jumla (Halisi)** | **11,644,678.37** | **14,225,435.73** | **12,603,012.29** | **88.59** | **8.23** |

*Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mei, 2018*

## JEDWALI NA 5: MALENGO NA MAKUSANYO HALISI

## KATIKA KIPINDI CHA MWEZI JULAI 2017 – APRILI 2018 (Zanzibar)

***Shilingi milioni***

| Idara | 2016/17 | 2017/18 | | | Asilimia ya Ukuaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | Makusanyo Halisi | Lengo | Makusanyo Halisi | Ufanisi (%) | |
| Kodi za Ndani | 66,099.50 | 84,909.40 | 91,708.50 | 108 | 38.74 |
| Ushuru wa Forodha | 103,487.60 | 129,059.80 | 118,552.10 | 92 | 14.56 |
| **Jumla** | **169,587.10** | **213,969.20** | **210,260.60** | **98** | **24** |

*Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mei, 2018*